GAZETI LA KWANZA LA ISLAM KUTOLEWA KWA LUGHA YA KISWAHILI - MWAKA 1936

AHMADIYYA MUSLIM JAMAAT TANZANIA

Mapenzi ya Mungu

MAPENZI KWA WOTE BILA CHUKI KWA YEYOTE

JUZU NO. 237 **MUHAR-SAFAR** 1444-5 **AH** **AGOSTI** 2023 **ZAHOOR** 1402 **HS** **BEI TSH 800/=**

Sherehe za Karne zaipamba Lajna Ijitimah

Ukurasa wa 3..

Na. Mariam Mahmood Mubiru
Dar es Salaam.



Sherehe za Karne zilikiambatana na ufunguzi wa Ofisi za Lajna Imaillah Tanzania, zilizofunguliwa na Maulana Sheikh Tahir Mahmood Chaudhry Sahib Amir na Mbashir Mkuu pamoja na SadrMajlis Lajna Bi. Zena Nyange Sahiba.

Ijtimaai MKAT 2023 kufana Dar es Salaam

Ukurasa wa 4..





Mgeni rasmi Maulana Sheikh Tahir Mahmood Chaudhry Sahib akiongoza zoezi la ugawaji wa zawadi katika kuelekea Rahim Jamil Mwanga Sahib, Sadr Majlis Kuhuddamul Ahmadiyya Tanzania

>UK .5 Mjadala wa Nguruka 20-21 May 2002

Ijtimaa za Kidini >UK .3

Mapenzi ya Mungu

Maoni ya Mhariri

Karne moja ya Lajna Immaillah (1922 - 2023)

Sifa zote njema ni za Allah Mtukufu aliyeijaalia na kuibariki tanziim ya Lajna Imaillah kusheherekea neema ya kutimiza karne moja toka ilipoanzishwa na Khalifatul Masih wa pili Hazrat Mirza Bashir-u-din Mahmud Ahmadra Mwaka 1922.

Kwa jitihada kubwa na weledi chini ya Sadri Lajna Zena Nyange na Majlis yake ambazo zote hizi ni zawadi za Allah. Lajna Immaillah iliandaa,ikaratibu,ikaendesha na hatimae kufanikisha sherehe zilizofikia kilele chake katika viwanja vyetu vya Kitonga. Alhamdulillahi Rabbil A'lamiin. Maandalizi yaliyofanywa katika matawi kuwatembelea wagonjwa, kusafisha mazingira na kuwasaidia wasiojiweza. Mahudhurio makubwa ya wana Lajna walijitokeza Kitonga. Mashindano ya kielimu yaliyoendeshwa kwa mafanikio makubwa; zawadi zilizotolewa kwa wale waliochangia kufanikisha sherehe hizo.Yote haya ni alama ya kukomaa kwa Tanzim hii muhimu katika Jamaat Ahmadiyya.

Katika kipindi hiki cha karne moja Tanzim ya Lajna daima imesukumwa na falsafa ya daima kwenda mbele akina mama kwa ushujaa mkubwa, wamesimama imara katika kulinda imani yao huku wakisimama na waume zao kupambana na misukosuko na upinzani ulioletwa na maadui. Historia ya Ahmadayya Tanzania inakumbuka kwa heshima kubwa michango ya akina mama wa Nyipara-Rusenda, Tabora na Njinyo jinsi walivyo shikamana na waume zao wakati wa jua kali na masika ili kulinda imani zao. Hawakuteteleka wala kurudi nyuma. Na sote tunafahamu ya kwamba katika kila mafanikio ya mwanaume nyuma kuna mwanamke.

Kazi kubwa imefanywa na Lajna katika kuwalea watoto katika maadili ya Kiislamu. Hii ni kazi kubwa kwani wakati mwingi watoto wako chini ya ulenzi wa mama na ndio maana Mtukufu Mtume Muhammadsaw amesema pepo ipo chini ya mama. Kazi kubwa ya malezi ndio imetupatia wanajamaati walio imara.

Lajna Immaillah wameshiriki kikamilifu katika kueneza ujumbe wa Allah. Wapo walioandika mashairi kuandika makala, kuendesha vipindi MTA kujitolea katika kufundisha Shule yetu ya Sekondari Kitonga.Na wapo waliouza mapambo yao ili kusaidia ujenzi wa msikiti. Kazi hizi wamezifanya bila mbwembwe bali kwa Staha wakitaka tu kupata radhi za mola wao.

Lajna Immaillah hawakukubali kuwa nyuma kielimu yamepatikana maendeleo makubwa katika uwanja wa elimu, wanaendesha madarasa ya Quran Tukufu na ni vizuri ikumbukwe kuwa,Lajna Immaillah ilitoa mchango mkubwa katika ujenzi wa Sekondari Kitonga ofisi zao walizotoa kwa Shule, akina mama wametoa michango katika ujenzi wa Shule na kwa hivi sasa kwa msaada wa Allah tunao wataalamu katika nyanja mbalimbali. Tunao Waalim, Madaktari na Wanasheria ambao wote hao wameiongezea heshima na sifa jamaati yetu. Lakini la msingi kuliko yote katika kufaulu kwao huko hawakusahau asilani mila na desturi ya Islam ya uvaaji wa Hijabu. Hakuna jambo la fahari kama kuutangazia ulimwengu mimi ni Mwislam.

Mafundisho yote haya yametokana na Lajna Immaillah kutekeleza maagizo wanayoyapata kutoka kwa kiongozi wetu mpendwa Hazrat Mirza Masrur Ahmadatba. Ni mwenendo utakao wa jaalia Inshaallah kupanda vilele vya mafanikio.



QUR'AN TUKUFU

(وَلَمَّا بَلَغَ أَشُدَّهُ آتَيْنَاهُ حُكْمًا وَعِلْمًا ۚ وَكَذَٰلِكَ نَجْزِي الْمُحْسِنِينَ) (يوسف:23)

Na (Yusuf)alipobalehe kikamilifu Tukampa hukumu na ilimu. Na hivi ndivyo Tunavyowalipa watendao mema.



NUKUU YA HADITHI

صحيح بخارى

كتاب: العلم ، مُعَاوِيَةَ خَطِيبًا، يَقُولُ: سَمِعْتُ النَّبِيَّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ، يَقُولُ: مَنْ يُرِدِ اللَّهُ بِهِ خَيْرًا يُفَقِّهْهُ فِي الدِّينِ، وَإِنَّمَا أَنَا قَاسِمٌ وَاللَّهُ يُعْطِي، وَلَنْ تَزَالَ هَذِهِ الْأُمَّةُ قَائِمَةً عَلَى أَمْرِ اللَّهِ لَا يَضُرُّهُمْ مَنْ خَالَفَهُمْ حَتَّى يَأْتِيَ أَمْرُ اللَّهِ.

Hazra Mua'wiya alisema akihotubia kuwa, mimi nilimsikia Mtume[saw] akisema: Mwenyezi Mungu akimtakia mtu heri basi humpa ufahamu wa Dini. Na mimi ni mwenye kugawa tu na Allah Mtukufu hutoa, na umma huu utadumu kusimama juu ya amri ya Allah Mtukufu wala hatawadhuru anayehitilafiana nao mpaka ifike amri ya Allah Mtukufu.



Nukuu ya Masih Aliyeahidiwa[as]

Umuhimu wa Kumfuata Mtume[saw]

Hazrat Aqdas Masihi Mau'udi a.s anasema: Tazameni, Mwenyezi Mungu Anasema ndani ya Quran Tukufu: Kwa ajili ya kuwa mpendwa wa Mungu Kuna njia moja tu ya ufuasi wa Mtume s.a.w na hakuna njia nyingine yoyote ya kukuunganisheni na Mungu. Lengo la Mwanadamu lapaswa kuwa tu kumtafuta Mungu mmoja asiye na mshirika. Yapaswa kujiepusha na shirki na bidaa. Haipaswi kuzifuata mila na kuzitii tamaa za nafsi. Tazameni! Ninasema tena kwamba mbali na njia ya kweli ya Mtume wa Allah s.a.w, Mwanadamu hawezi kwa vyovyote vile kufanikiwa.

Mtume wetu ni mmoja tu, na Quran Tukufu moja tu iliyoteremka kwa Mtume huyu, ambayo kwa kuifuata twaweza kumfikia Mungu..... Kumbukeni kwamba hakuna ufunguo mwingine wowote ule wa kufungulia milango ya fadhili na baraka za Mungu pasipo kufuata maagizo ya Quran Tukufu na Mtume s.a.w na Sala na Saumu, ambazo ndizo njia za SUNNA. Amepotea yule aziachaye njia hizo na kubuni njia yoyote nyingine mpya. Atakufa bila mafanikio yule asiyefuata maagizo ya Mungu na Mtume wake bali anatafuta njia nyingine. Malfudhat J. 3, uk. 102 - 103, toleo jipya.

Mwezi wa Muharram na Sala ya Mtume[saw]

Khalifa wetu wa tano Hazrat mirza Masroor Ahmad atba anasema:" kama Muharram inatutolea darasa lolote basi ndilo hilo kwamba, tuendelee kumsalia Mtume[saw] na A'ali yake daima dawamu. Tuendelee kujitahidi kwa ajili ya kutimiza wajibu wetu wa kuyapata makusudio ya Imamu wa zama kuipitia sala ya mtume na maombi na tusimame kidete tukionesha uimara mbele ya watu wenye tabia ya kiyazidi. ***(Khutbate Masroor.J.8.uk.636)***

BODI YA UHARIRI

Msimamizi: Sheikh Tahir M. Chaudhry - Amir Jamaat, Tanzania.
Mhariri: Dr. Swaleh Kitabu Pazi
Kompyuta: Jabiri Faraji Bishazo.
Mchapishaji: Sheikh Raghib Zia ul Haq
Msambazaji: Mwl. Omari Ali Mnungu
Wajumbe: 1. Mwl. Abdullah Khamis Mbanga
2. Mahmood Hamsin Mubiru.
3. Jamil Mwanga.
4. Abdillah Kombo

Makao Makuu - Ahmadiyya Muslim Jamaat Tanzania,
Mtaa wa Bibi Titi Mohammed, S.L.P. 376.
Simu 022 - 2110473, Fax 022 - 2121744, Dar es Salaam, Tanzania.
Email: mapenziyamungu36@gmail.com

I j t i m a a z a K i d i n i

Dini tukufu ya kiislamu ambayo inadai kuwa dini ya asili, ikizingatia umuhimu wa mkusanyiko wa kidini, inawafundisha wafuasi wake kukusanyika pamoja mara kwa mara ili waweze kuendesha maisha yao kwa njia iliyo bora. Kila siku waislamu wanakusanyika mara tano msikitini kwa ajili ya sala kisha wanakusanyika katika msikti mkubwa kwa ajili ya Ijumaa, tena wanawake kwa wanaume wanakusanyika mara mbili kwa mwaka kwa ajili ya Idi katika eneo kubwa zaidi, kisha kuna mkusanyiko wa Hija ambao unaweza kuitwa mkusanyiko mkuu wa kidini wa mwaka duniani.

Waislamu wanaposhiriki katika mikusanyiko hiyo, kwanza wanafuata aya hii ya Kurani tukufu كونوا مع الصادقين yaani wanapata nafasi ya kukaa na watu wema. Wanajifunza mambo mbalimbali kutoka kwa ndugu zao. Uongozi nao unawafunza mambo mengi na hao watu wanaporudi kwenda nyumabi kwao, wanarudi wakiwa wamejifunza elimu ya kidini na desturi njema ambazo watawafundisha wenzao wasioweza kuja kutokana na udhuru fulani fulani. Ndiyo sababu tunaona nidhamu na desturi za aina moja katika ulimwengu wa kiahmadiyya duniani kote.

Khalifa mtukufu wa tano, Hadhrat Mirza Masroor Ahmad aba akiwasihi wanajamati alisema " Siku hizi tatu za Ijtimaa zisiwe sababu ya mabadiliko ya muda ndani yenu bali jitahidini kuleta mabadiliko ya kudumu katika nafsi zenu, nyanyueni viwango vya uchamungu na ibada, mvuto mbaya wa Magharibi usiwe chanzo cha kuwavuta kwake. Daima mkumbuke kujitolea kwa ndugu zenu wale ambao wakiimarisha imani yao, wanafanya kila jitihada kunyanyua juu bendera ya Ahmadiyya yaani Islamu ya kweli na wanajitolea kwa kila namna kwa kutimiza ahadi zao" (Hotuba ya Ijumaa, 24/9/2010)
Mwenyezi Mungu Atujalie tufaidike na nafasi hizo na kuingia katika kundi la watu ambao kuhusian nao imeelezwa katika Hadithi kuwa Mwenyezi Mungu Ametangaza kuwasamehe wale wote waliomo katika mkusanyiko wa kumkumbuka Yeye. Amin

Sherehe za Karne zaipamba Lajna Ijitimah

Kwa fadhila za Allah, Tanzim ya Lajna Imailah imehitimisha Ijitimaa yake ya kila mwaka iliyofanyika katika viwanja vya Jamaat vilivyopo Kitonga jijini Dar es Salaam. Shughuli mbalimbali za Jumuiya hufanyika hapa kwa nafasi ya kutosha (Alhamdulillah).
Mara kwa mara niwapo katika viwanja hivi mawazo yangu huenda mbali na hukumbuka muasisi wa maeneo haya bwana **Ali Saidi Mosse Sahib**, Amir Jamaat Tanzania (2006 – 2009) Allah ampokelee juhudi zake na kumrehemu. Kitonga sasa yafana sababu ya Ahmadiyya.
Ijitima hii ni ya kipekee kwani imeambatana na maadhimisho ya Karne 1 toka kuanzishwa kwa Tanzim hiyo ya Lajna Imailah na Khalifatul Masih wa pili wa Seyidna Ahmad[as] Hazrat Mirza Bashirdin Mahmood Ahmad[ra] mnamo mwaka 1922. Lajna Imailah ni Tanzim kwa ajili ya watumishi wa Allah wa kike walio juu ya miaka 15 na lengo haswa la kuanzishwa kwake ni kuwapa sauti wanawake katika uongozi kwenye jamii zao na uwezo wa kutimiza wajibu wao.
Lengo haswa la Ijitima ya Lajna ni kuwaleta pamoja akina Mama wa Kiahmadiyya ili wafaidi upepo wa kiroho wa kuwa pamoja, kuzidisha uchamungu, kuongeza elimu ya Dini na kuongeza



mshikamano wa umoja.
Allah anatueleza katika Quran Tukufu, 'na katika usiku, pia amka (uisome) ndiyo ibada zaidi kwako, huenda mola wako akakuinua cheo kinachosifika (Sura Banii Israiil 80), nasi tunafuata muongozo huu kwa kuamka kwa ajili ya Sala ya Tahajjud kama ufunguzi wa ratiba yetu ya siku katika Ijitimaa yetu. Ibada hii ni neema hasa na zawadi itokayo kwa Allah ambayo humfikisha mtu kwenye cheo kikubwa cha heshima sana. Swalatul Fajr hufuatia, Darasa la Quran Tukufu, ufafanuzi wa masharti ya Biat kisha mazoezi ya viungo.
Mazoezi ni jambo la muhimu na ni katika mienendo ya viongozi wetu wa kiroho, Mtume saw mbora wa viumbe alisema; muumini mwenye nguvu ni bora na anayependwa na Allah kuliko mdhaifu na kuna wema katika wote (Sahihi Muslim). Yeye Mtume[saw] alihama kutoka Makka kwenda Madina akisafiri takriban Maili 338 chini ya Jua kali na linalochoma. Aliwahimiza akina Baba kuwafundisha watoto kuogelea, kutupa Mishale na kupanda Farasi na yeye alikuwa bingwa wa kupanda Farasi bila hata hatamu. Kwa upande wa Masih wake, Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad[as] mara kwa mara alikuwa akitembea kwa haraka sana baada ya Swalatul Fajr na wakati mwingine jioni, haya ndio yalikuwa mazoezi yake ya mara kwa mara na yaliendelea katika maisha yake yote. Mitume wa Mwenyezi Mungu walikuwa wanaviweka Viungo vyao kwa mazoezi na si kwa ajili ya upuuzi bali kwa ajili ya Ibada.

Kikao cha kwanza cha Ijitimah kilifunguliwa rasmi kwa usomaji wa Quran Tukufu, kiapo cha Lajna kilichoongozwa na Sadr Sahiba, shairi kisha khutba fupi ya Sadr kumkaribisha mgeni rasmi Naib Amir Maulana Sheikh Abdurahman Ame Sahib kwa ufunguzi na maombi.
Kama dini yetu Tukufu inavyotufunza ya kwamba tushindane katika wema, mashindano ya kielimu yalifanyika katika nyanja mbalimbali kuhifadhi Quran, kusoma Quran na tafsiri, hotuba, maswali na majibu pamoja na mashindano ya kimichezo.
Waswahili husema utavuna ulichopanda, washindani wote wa mashindano ya kielimu waliopanda nanasi walivuna nanasi halikadhalika waliopanda korosho walipata sawia. Tuzo mbali mbali zilitolewa pia katika nyanja mbali mbali wafanyakazi bora, wanafunzi waliofanya vizuri katika masomo, waliojitolea kwa hali ya kijamii au kidini na Masadr wote waliopita pia walipatiwa tuzo.
Kwa msaada wa Allah Ijitimaa yetu ilitamatika kwa mafanikio makubwa na kikao kufungwa na Naibu Amir Sheikh Abdurahman Ame kwa nasaha na maombi ya pamoja kama ilivyo desturi yetu.
Tarehe 17.06 ndiyo siku iliyosubiriwa kwa hamu na gamu na Lajna wote, ndiyo siku kubwa katika historia ya Tanzim yetu Bila ya shaka sisi pamoja na vizazi vyetu hatutakuwepo tena baada ya miaka 100 ijayo kuadhimisha karne ya pili.
Juhudi kubwa ilifanywa na Lajna na Nasrat nchini kote ikiongozwa na Sadri wetu Bi. Zena Nyange Sahiba katika kufanikisha Sherehe hizi za karne, shughuli mbalimbali za kijamii zilifanyika katika kuliendea jambo hili la kuadhimisha miaka 100 ya Tanzim yetu hii adhim, kutembelea Wagonjwa, Magereza, Watoto Yatima, kusafisha maeneo ya Uma, kuchangia Damu, kugawa vipeperushi na vitabu vyenye ujumbe wa jamaat, kupanda miti pamoja na kutengeneza Kanga zenye kumbukumbu ya maadhimisho haya huku jina la Kanga likiwa limetoka kwa kiongozi wetu mpendwa Hazrat Mirza Masroor Ahmad (aqdas), na jina alilolichagua ni "kuwa na haya ni sehemu ya Imani".

Ufunguzi wa sherehe hizi za karne ulipata Baraka ya kufunguliwa rasmi na Amir Sahib Maulana Sheikh Tahir Chaudhry sambamba na kuzinduliwa jengo la Lajna lililojengwa kwa michango iliyotokana na Tanzim yetu pekee.
Lajna wakijipamba kwa mavazi meupe ishara ya amani huku Nasrat wakivalia nusu kanzu za rangi ya bluu kwa mitandio meupe, hakika ni furaha, amani na upendo ndio lugha ya picha iliyojidhihirisha katika mkusanyiko ule…Hakika ni miaka 100. Hakika ni karne 1! Sote kwa baraka za Allah tulikuwa chini ya kivuli cha mapenzi kwa wote bila chuki kwa yeyote.
Kutimia kwa karne moja si kitu kidogo na bila ya shaka kumeambatana na maendeleo makubwa katika Tanzim hii. tunapaswa kufahamu wanawake wa kiahmadiyya wana uongozi wao (Majlis Amila) ambao wanashughulikia mambo ya fedha, elimu, afya na mazoezi, mambo ya kijamii, kutoa majarida na kadhalika yahusuyo Tanzim hiyo. Matawi ya mikoani yanaunganishwa na makao makuu. Kila Tawi lina kiongozi wake, kitaifa kiongozi ni Sadr anayehidhinishwa na Huzur. Lajna pia wanashiriki katika Majlis Shura kupitia mwakilishi wao.
misikiti minne imejengwa kwa kutumia michango ya wanawake wa kiahmadiyya mpaka kufikia 2008, (www.reviewofreligion.org) wanawake wa kiahmadiyya ambao ni wasanifu majengo wameshiriki katika kusanifu na ujenzi. Kwa fadhila za Allah Lajna Imailah Tanzania imefanikiwa kuchapisha kijalada chake kiitwacho Nusrat mwaka jana Mwezi wa 8.
Jengo la Lajna Kitonga lilitoa mchango mkubwa katika kuanzisha kwa Shule ya Sekondari Kitonga na takwimu zinaonyesha Lajna hawakua nyuma katika michango ya kusimamisha shule hiyo.
Gazeti la Misbah lilianzishwa mwaka 1926 mahususi kwa ajili wakina Mama wa Jamaat ingawa kulikuwa na changamoto za kifedha. Nusrat Girls High School ilianzishwa mwaka 1928 Qadian ili mabinti wapate nafasi ya kielimu na mwaka 1951 chuo cha wanawawake kilianzishwa Rabwah.
Mafanikio ya Lajna yanajidhihirisha pia katika mchango wao kwa kuwasaidia akina Baba kusimama imara wakati ulipoingia msukosuko wa kunyang'anywa wake. Ilikuwa mtihani mkubwa na mbinu ya kuwatikisa waaminio. Mifano ya kungara ilijitokeza huko Rufiji, Njinjo na Tabora. akina Mama walisimama Kotini kuwatetea waume zao na kusema kwamba toka waolewe ndio sasa wanatimiza barabara mafundisho ya Islam. Kabla ya hapo, walikuwa wanacheza ngoma na kushiriki mambo ya kishirikina.
Akina Mama wamejitokeza katika makala katika Mapenzi ya Mungu wakitoa makala juu ya Malezi, Mapishi na Utunzi wa Mashairi. Binti Rafia ameandaa kitabu kuhusu Ukhalifa wa Kiahmadiyya ambacho hakijachapishwa. Akina Mama wa Songea ukoo wa Farock na Varda waliuza mapambo ya Dhahabu ili kujenga Msikiti wa Songea.
Lajna walishiriki kikamilifu katika kuwalaki Makhalifa na walii ambao wameitembelea Tanzania. Khalifatul Masih wa 4 [rh] alikutana nao na Khalifatul Masih wa 5 [atba] walioshughulika na upikaji wa chakula ni Lajna.
Mafanikio haya yote yanahitaji kujitolea kifedha kama tunavyojifunza katika Quran Allah anaposema ***'Wale wanaotoa mali zao katika njia ya Mwenyezi Mungu kisha hawafuatishii waliyoyatoa masimbulizi wala udhia, wao wana ujira wao kwa Mola wao, wala haitakuwa hofu juu yao wala hawatahuzunika (2:263)'***
Syeda Nusrat Jahan Begum[ra] mke wa muanzilishi wa Jumuiya ya Waislam wa Ahmadiyya alikuwa mstari wa mbele kujitolea kifedha. Mwaka 1900 Masih Aliyeahidiwa alidhamiria kujenga Mnara mweupe katika kijiji chake cha Qadian yalipokuwa makao makuu ya Jumuiya ili kutimiza bishara ya Mtume[saw]. Aliwaomba Wanajamaat kuchangia Rupia 10,000 kukamilisha mradi huo na kushauri katika Wanajamaat 100 kila mmoja akichangia Rupia 100 mradi utafanikiwa. Mke wake bila kusita aliuza miliki yake alilorithi iliyokuwa maeneo ya Delhi na kuchangia Rupia 1,000 kwa ajili ya ujenzi wa Mnara na hivyo kuchangia 1/10 ya gharama za mradi.
Mbali na kujitolea kifedha Lajna Imaillah Tanzania tunatakiwa kujitathmini na kuelewa dhumuni haswa la kuwa na Tanzim hii, miaka 100 ya kusheherekea toka kuanzishwa kwa Tanzim hii kuambatane na utekelezaji kwa vitendo. Kila mmoja kwa nafasi yake aangalie, apime na arekebishe pale anapoona hajakamilisha wajibu wake. kama tunataka msaada wa Allah utushukie kutoka mbinguni na malaika watufunike kwa mbawa za huruma basi yafuatayo yatekelezwe kwa shughui. Nayo si mengine bali ni maazimio ya Tanzim hii

- Kutafuta elimu lakini kipaumbele kikiwa uchamungu
- Kuhudumia jamii kwa kutumia nguvu kazi na ujuzi tulionao na kuhamasisha michango kwa ajili ya kusaidia wenye mahitaji.
- Kuwalea watoto ili waishi maisha yanayopendekezwa na Islam.
- Kuhamasisha umoja, mshikamano, kuvumiliana kutokana na udhaifu wa kibinadamu
- Kupambana na matatizo yote kwa bidii na ushujaa
- Kuwasaidia Masikini.

Bila ya shaka tukitekeleza haya , msaada wa Allah utashuka kutoka mbinguni na kupata mafanikio makubwa katika Tanzim yetu na jamii kwa ujumla kwa kutengeneza kizazi chenye wema hapo baadae.
Kila lililo na mwanzo huwa na mwisho, Lajna Imailah tumeandika Historia, tumefanikisha jambo letu kwa ukubwa na muitikio wa washiriki 1251 kutoka mikoa 19 nchini, matawi 111 wakiwemo Lajna 561, Nasrat 472, Atfal 143 na Wageni 75. Bila ya shaka muitikao huu wa washiriki ni kwa baraka za maadhimisho haya ya karne moja.
Kwa msaada wa Allah sherehe za karne zilifungwa rasmi na Amir na Mbashir mkuu sambamba na tuzo mbalimbali kutolewa kwa waliojitolea kufanikisha sherehe hizi za karne.

Ijtimaai MKAT 2023 kufana Dar es Salaam

Mashindano ya Kielimu, Kimwili yachagiza mafanikio makubwa

Na:
Isihaq Nyamihasi,
Dar es Salaam.

Kwa fadhili na Rehema za Allah Mtukufu, Majlis Khuddamul Ahmadiyya Tanzania ilifanikiwa kufanya Ijtmaa yake ya Khuddam na Atfal Kuanzia Tarehe 23 hadi 25 June katika viwanja vya Ahmadiyya Kitonga Jijini Daressalaam, huku wahudhuriaji kutoka mikoa 16 ya bara



na visiwani wakihudhuria.
Ijtmaa hiyo ya 33 nchini Tanzania ilifanikiwa kwa kiasi kikubwa ikiwa na washiriki wengi wakiwa ni pamoja na Khuddam 255,Atfal 167 na Ansarullah 13 waliotimiza idadi ya washiriki 435 Alhamdulillah.
Katika siku ya kwanza ya mkutano huo, washiriki walifanikiwa kuswali swala ya pamoja ya Ijumaa, kisha kupata chakula cha mchana kwa pamoja tukio lililofuatiwa na ufatiliaji wa hotuba ya Ijumaa ya Kharifatul Masihi V Hadhrat Mirza Masroor Ahmad[atba]. Kupitia **MTA**





Pia katika siku hiyo ya kwanza wahudhuriaji walipata wasaa wa kusikiliza ujumbe wa Ijtmaa hiyo kutoka kwa Khalifa Mtukufu[atba] uliosomwa mbele yao na Sadri Majlis Khuddamul Ahmadiyya Tanzania ndugu Rahim Mwanga, kabla hajatoa hotuba ya ufunguzi rasmi wa Ijtmaa uliofatiwa na maombi ya kimya kimya kwa washiriki wote.

Kupitia hotuba yake, Sadr Sahib Majlis Khuddamul Ahmadiyya Tanzania aliwasisitiza Khuddam wote nchini kutoa muda wao kushiriki matukio mbalimbali ya Jamaat Ahmadiyya Tanzania na yale ya Tanzeem, pia kujitahidi Kuimarisha uhusiano wetu na Khilafat kwa Kumuandikia barua kiongozi wetu Mpendwa Hadhrat Khalifatul Masih V[atba] na kuhakikisha tunafatilia hotuba zake kila Ijumaa.

Mashindano mbalimbali ya kielimu na kimwili yaliendelea kwa siku zote tatu, yakiongozwa na Mashekh na Waalimu mbalimbali waliokuwepo katika Ijtmaa hiyo yakilenga kukuza uelewa wa masuala ya kidini hasa masomo ya Dini. Sala ya kiislamu na usomaji wa Qur'an Tukufu kwa Khuddam na Atfal wote, huku washiriki wakipata wasaa wa kushiriki Swala zote, Chakula na Malazi kwa pamoja.









Sambamba na Hayo hotuba mbalimbali zilitolewa. Kwa fadhili za Allah siku ya Jumapili ya Tarehe 25 Juni, Mheshimiwa Amir Jamaati na Mbashiri Mkuu Shekh Tahir Mahmood Chaudhry Sahib, aliweza kufika na kutoa ujumbe wake kwa Khuddam na Atfal wote nchini huku akiwapongeza kwa kuacha shughuli zao na kufika katika tukio hilo adhimu la kitanzim. Kisha aliongoza maombi ya kimya kimya na kufunga Ijtmaa hiyo rasmi kwa mwaka huu na kuwaomba washiriki kujiandaa na Ijtmaa inayofata ya mwakani 2024 Inshaallah.
HAKIKA IJTMAA ILIFANA!!.



Mjadala wa Nguruka 20-21 May 2002

Na.
Hassan Sango (Makamu M/kiti)
Mjadala wa Nguruka, Kitonga.

Kwa fadhili za Mwenyezi Mungu ulifanyika Mjadala wa kihistoria uliofanyika NGURUKA katika mkoa wa Kigoma.

Chanzo chake ilikuwa wakati Mzee Moshi Muhammad Mlekyakule alipokuwa chama cha NCCR Mageuzi, alipokuwa katika harakati za siasa alikuwa karibu sana na aliyekuwa mbunge wa jimbo la Kigoma Kusini Kifu Ghulam Hussein Kifu. Alimfukishia ujumbe wa Masih wa Mtume Muhammad saw kwa muda na akampatia CD yenye mjadala uliofanyika TANGAMANO TANGA. Kati ya Sheikh Bakr Kaluta wa Jumuiya ya Waislam wa Ahmadiyya na Sheikh Abdul Qadir Adinan.

Ambayo Sheikh upande wa Sunni alionekana kushindwa, baada ya kuona mheshimiwa mbunge alitilia shaka kama kweli Sunni walishindwa au ni Ahmadiyya watupu wanaigiza mmoja akijifanya Sunni mwingine Ahmadiyya ili Sunni aonekane kashindwa.



Pichani ni Maulana Sheikh Ahmad Dadi Mmoto akishiriki katika Mjadala wa Nguruka Kigoma.

Pia akatoa ushauri kuwa tumeishaongelea swala hili kwa muda mrefu baina yake na Mzee Moshi. Hivyo anataka waitwe Masheikh wakubwa kwa sababu utakapofanyika mjadala wa watu wa Nguruka watakaposhindwa watasema kwa sababu elimu yao ni ndogo.

Baadae alifanya mpango na Masheikh Kigoma Mjini wakakubali. Akamueleza Mzee Moshi kuwa, nimeshakubaliana na Masheikh, sasa nyie Ahmadiyya mmefikia wapi? Maana nisingependa Masheikh wangu waje alafu wa kwenu wasitokee.

Mzee Moshi akamwambia kuwa nimekwisha peleka ujumbe makao makuu Dar es Salaam, nimehakikishiwa kuwa watakuta sina wasiwasi.

Ndipo Mheshimiwa Mbunge alipoamua kutoa Shilingi za Kitanzania elfu kumi (10,000.) kama mchango wake wa nauli nasi tuchangie zilizobaki ili atumwe Mjumbe maalum kwenda Dar es Salaam kufikisha ujumbe tena wa Mjadala.

Baada ya Waahmadiyya kuchanga fedha iliyobaki na kushawishi Mzee Moshi Muhammad alichaguliwa kuwa mjumbe.
Alipofika Dar es Salaam Sheikh alimhakikishia safari ya kuja Nguruka ipo pale pale na si hivyo tu, bali alinunua vipaza sauti kwa ajili ya Jamati ya Nguruka.

Nyuma ya Pazia

Baada ya kufanyika Mjadala na kwa kutokuelewa au Hila Mzee Kapenta Kasisiko akatangaza kuwa upande wa Sunni umeshinda bila kuhakikisha wameshindaje.

Jamaa wa Sunni walijilazimisha kushangilia, katika harakati zao waliamua kuonyesha mjadala huo kupitia video walizoteua. Wamezirekodi ili kuwaonyesha waumini wao kuwa, kweli Ahmadiyya wameshindwa. Kilichotokea jenereta za kuonyeshea ziliungua na umati uliokusanyika haukushuhudia chochote.

Masheikh waliotokea Kigoma yaani Mzee Kitama Ibrahim, Sheikh Abdul-Razack na wengine. Walichukua CD zile ambazo watu wa Nguruka walishindwa kuona kutokana na kuungua Mashine kwa ahadi kuwa watazikopi na kuzirudisha toka mwezi wa 5/2002 mpaka leo 2023.
Huu ni ushahidi tosha kuwa hakika waliogopa aibu yao kuonekana.
Baada ya Mjadala Mzee Moshi Muhammad alifika Ujiji kwa Mzee Kitama Ibrahim ambaye baada ya mazungumzo alimwagiza Sheikh Mtoto ambaye ni mtoto wake ili Mjadala ufanyike tena, jibu alilorudishiwa ni kwamba wale Masheikh wamekataa kufanya mjadala na Ahmadiyya, Mzee Kitama kama anataka afanye mwenyewe mjadala.

Mjadala kwa waliotaka kuficha akina Kitama na wenzake kwa Fadhili za Allah unapatikana kwenye YOUTUBE. Kwa wale wenye simu janja unaweza ukaandika neno NGURUKA au Ahmadiyya vs Sunni au Mihadhara ya Kiislamu, wanasema kusikia ni sawa na kuona, ndio maana sikutaka kuandika yaliyozungumzwa kwenye Mjadala fuatilia ili upate ladha hiyo.

Maulana Sheikh Muzaffar Durran alipotembelea Tanzania wakati wa Mkutano wa Ahmadiyya Tanzania (Jalsa Salana ya 50) alipoulizwa kuhusu Mjadala wa Nguruka alijibu ule ulikuwa ni msaada maalumu kutoka kwa Allah

Kwa hakika kweli walichosema Masheikh, badala ya kuuliza ni kwa ushahidi gani utume unaendelea, wao walianza kuhoji yaliyosemwa na Waahmadiyya kabla ya wakati, lakini pia walikuja na vitabu vingi na wakashindwa kuvitumia.

Ajabu Iliyotokea

1. Baada ya Mjadala, hakuna tena Sheikh aliyejitokeza akitaka Mjadala. Sasa miaka Ishirini imepita.
2. Mzee Kitama (Mwanamgambo) hajui Kiarabu akawa mzungumzaji mkuu. Wakati Masheikh wanadai kama hujui Kiarabu hujui Dini. Wanaojua Kiarabu kama Sheikh Rizik Abdul Razak na Sheikh Daud Kasoma hawa kwao na uwanja mkubwa wa kuongea.
3. Ansar Sunni wa Kigoma wanaamini Nabii Issa[as] kisha farikina wao wanaamini sana Hadith na kutoka katika Bukhar na Muslim kuna hadith zisemazo Nabii Issa[as] atarudi na vitabu hivyo ni sahihi. Sasa atarudi vipi? Kama sio ujaji wa Issa wa mfano kama ujio wa Eliya kutimizwa na Yohana (Yahya[as]). Hivyo mwanzilishi wa Jumuiya ya waislamu wa Ahmadiyya Mirza Ghulam Ahmad[as] ndio Issa alitajwa na Mtume [saw] kurejea. Mwenye Masikio na asikie.

Kwa sababu ya Maulana Sheikh Durrani baada ya kuagiza habari za mjadala ziandikwe tena na pia ndugu wengine kuniuliza mara kwa mara kuhusu Mjadala huu. Kwa fadhili za Mwenyezi Mungu namshukuru kuniwezesha kuandika haya.Na neno langu la mwisho sifa zote zinamhusu Mwenyezi Mungu.

Bustani ya Washairi

Tusizibeze Kufanya Shughuli za Jamaat

NIDHAMU kitu azizi, kwenye wowote Umoja
Muhimili na mizizi, wa kile mlichochuja
Kitaenziwa makuzi, na kuendeshwa kitija
Shughuli za Jamaati, tusizibeze kufanya.

Kwenu wanajamaati, majina sita yataja
Bali nyote jumlati, ipokeeni lihaja
Waume na mabinati, wito huu unakuja
Tusizibeze kufanya, shughuli za Jamaati.

Wote ninawashauri, NIDHAMU kutoifuja
Bila hiyo ni khatari, bila hiyo kifo chaja
Hivyo kwa kujinusuri, tuwe nayo bila hoja
Shughuli za Jamaati, tusizibeze kufanya.

Huusikiapo wito, waitwa kwenye shughuli
Kusadi wajawazito, ama Wakala-Amali
Itika siwe mzito, wala kuuliza swali
Tusizibeze kufanya, shughuli za Jamaati.

Jua sisi wanajeshi, wakati wote kazini
«Leo ni vipeperushi», tunavigawa mjini
Tusitengeneze shushi, haipo kwenye kanuni
Shughuli za Jarmaati, tusizibeze kufanya.

Huhimizwapo kutoa, katika njia ya Mola
Mazao mifugo pia, wakadhaa kawarila
Uache kulimatia, toa upate fadhila
Tusizibeze kufanya, shughuli za Jamaati

Tunyoshe mikono yetu, viganja tusivifumbe
Tuzitoe mali zetu, Kondoo, Mbuzi na Ng›ombe
Ikibidi kila kitu, si vyetu ni vya Muumba
Shughuli za Jamaati, tusizibeze kufanya.

Patamkwapo twendeni, twendeni hospitali
Wagonjwa tuwaoneni, tukawajulie hali
Acha sababu kubuni, shiriki katika hili
Tusizibeze kufanya, shughuli za Jamaati

Na mmoja kati yetu, maradhi yakimpata
Wallahi tusithubutu, bila ya kwake kupita
Huyu ndiye ndugu yetu, tusimwache katakata
Shughuli za Jamaati, tusizibeze kufanya.

Tukamjulie hali, kama tunacho tumpe
Aende hospitali, gharama dawa alipe
Ndio udugu wa hali, na mali tusiutupe
Tusizibeze kufanya, shughuli za Jamaati

Tamati twakumbushana, unafaa ukumbusho
Hasa kwa wauminina, twafanya masahihisho
Tujisahihishe sana, tushike safi fundisho
Shughuli za Jamaati, tusizibeze kufanya

Al-Ustadh Mhenga
Khamisi S. S. Wamwera
Kimbangulile - Mbagala Rangitatu.
Dar es Salaam.

Wako wapi?

Baliwa waliotamba, bila wao hatushindi.
Mitaani wakiyumba, na kupita kwa makundi.
Wamekuwa ni wembamba, kusagika ja mahindi.
Masikini Binadamu, mwepesi wa utelezi.

Mahmood Hamsin Mubiru (wa Mamba)
Migombani-Kiwalani.

AHADI YA KIHISTORIA YA MWANA ALIYEAHIDIWA

Na jinsi alivyotekeleza ahadi ile

Kutokaa Uk wa 8..

Mau'ud sawa na utabiri ule uliotolewa na Masihi Aliyeahidiwa a.s. Na upande mwingine leo hakuna mtu ambaye anawajua wale ambao walikataa Ukhalifa. Na hii pia ni hisani ya Mwana Aliyeahidiwa kwao kuwa sisi waahmadiyya pekee ndiyo wanaowataja majina yao leo.

Kwa neema ya Mwenyezi Mungu zama za Ukhalifa wa Hadhrat Mirza Bashiruddin Mahmud Ahmad [ra] iliendelea zaidi ya nusu karne na ilijaa na matukio mengi ambayo yalihusu nyanja mbali mbali za mtu binafsi, za jumuiya, maisha ya kitaifa na kimataifa. Kubainisha historia yote ya zama za khalifa wa pili inahitaji muda yasiohisabika, kwahiyo nitajaribu kugusa baadhi ya mambo kwa kifupi yatakayoeleza utekelezaji wake wa ahadi ile aliyoifanya na Mwenyezi Mungu katika sura ya kutumikia haswa Islam Ahmadiyyat na kwa ujumla Ubinadamu.

Kwa mfano alianzisha, Gazeti la Al-Fazl, Tehrik-e-Jadid, Waqf-e-Jadid, Nidhamu ya Tandhim zote, Answarullah, Khuddam-ul-Ahmadiyya, Atfal-ul-Ahmadiyya, Nasira-tul-Ahmadiyya, Lajna Imaa'illah, Majlis Shura, Darul Iftaa; yaani chombo cha kupata fatwa kuhusu mambo mbali mbali yanayohusika dini, Darul Qadhaa; chombo cha kusuluhisha migogoro mbali mbali n.k. Ujenzi wa Mnara wa Masihi pia ulikamilika katika zama zake.

Katika kutekeleza ahadi ile alijitahidi sana, katika zama zake Jumuiya ilienea katika nchi takriban 70 na. Wabashiri waliandaliwa kisha walipelekwa katika nchi nyingi za bara zote.

Sasa nitajaribu kuweka mbele yenu muhtasari wa kazi zilizochapishwa za Mwana Aliyeahidiwa r.a.

Khalifa Mtukufu a.t.b. katika hotuba yake ya Ijumaa Tarehe 17 mwezi wa pili 2023 akielezea kazi zake na kusema; kwamba vitabu vyake, hotuba, mihadhara ya Mwana Aliyeahidiwa r.a, ambayo yamechapishwa katika mfumo wa kitabu au yako tayari kuchapishwa idadi zao ni 1,424. Zinapatikana katika muundo wa seti iitwayo Anwarul Uloom ambayo ina juzuu 38. Jumla ya kurasa ni 20,340.

Khalifa Mtukufu (aba) alisema; tukihisabu Tafsir-e-Kabir (Maelezo makubwa) na Tafsir-e-Saghir (Maelezo madogo) pamoja, jumla ya ukurasa zinazojumuisha kazi zake za Maelezoya Qur'ani Tukufu inafika ukurasa 28,735. Alitoa 1,808 Hotuba ya Ijumaa, ambayo ina kurasa 18,700. Alitoa Hotuba 51 za Eid al-Fitr ambazo zina kurasa 503. Alitoa Hotuba 42 za Eid al-Adha zenye kurasa 405. Alitoa hotuba 150 za Nikah, (yaani tangazo la ndoa) ambazo zina kurasa 184. Hotuba yake katika Mkutano wa Shura pia zimechapishwa ambazo zina kurasa 2,131. Kuna aina nyingine pia za maandishi yake zinapatikana, tukihisabu ukurasa zote za kazi zake, zinafikia kurasa 75,000. سبحان الله وبحمده سبحان الله العظيم

Khalifa Mtukufu (aba) alisema; imedhihirika kuwa Hazrat Musleh Mau'ud (ra) alikuwa na baadhi ya machapisho katika Al-Fazal na Al-Hakam ambayo bado hayajajumuishwa katika Anwarul Uloom. Kuna makala 55, hotuba 27, vipindi 43 vya maswali na majibu, kaulli zake 220 zilizorekodiwa, na barua 131 imepatikana hadi sasa.

Khalifa Mtakatifu (aba) alisema kwamba ameacha hazina kubwa ya kiakili. Sifa zote zilizotabiriwa kwa Masihi Aliyeahidiwa (as) kuhusu Mwana Aliyeahidiwa zote zilipatikana katika Hadhrat Mirza Bashiruddin Mahmud Ahmad (ra). Mungu alimpa elimu na ufahamu, kiasi kwamba hakuna mwanachuoni yeyote anayeweza kushindana naye au kulinganishwa naye. Kazi zake zote ni hazina kwa Jumuiya hii, na kazi kubwa inaendelea kufanywa kutafsiri kazi zake katika lguha ya Kiingereza. Khalifa Mtakatifu (aba) aliomba kwamba tufaidike na kazi hizi.

Mwishoni nitamaliza makala hii kwa maneno ya Hazrat Musleh Mau'ud r.a. Mnamo tarehe 28 Disemba 1961 alisema;

"Kama mtu yeyote anadhani kuwa mambo yote niliyoyafanya mimi kwa ajili ya kueneza Islam, Mungu Apishe mbali, ni mambo ya upuuzi tu… ndipo ninamwambia mtu huyu aje na ashindane, afanye kazi, kama kazi zake zitakuwa bora zaidi, basi dunia nzima itamfuata yenyewe… lakini kama kuna kundi fulani ambalo lina kazi yake ni ya kulaumu tu, watu hawa wakumbuke kwamba dunia hii sio bila ya kiongozi. Dunia hii ina Mungu ambaye ni Hai na mwenye nguvu zote. Wanaweza kunilaumu mimi, wanaweza kupanga mpango dhidi yangu mimi, wanaweza kunilaumu kwa lawama za uwongo, ili waweze kinifedhehesha katika macho ya watu wengine, lakini hawa watu kwa sababu ya mipango yao hizi katika matokeo hawawezi kujilinda nafsi zao kutoka mkono wa Allah. Anaendelea kusema; "Lakini mimi kwa kumtegemea Mungu yule yule natangaza kwamba jina langu daima litabaki duniani. Ingawa nitakufa, lakini jina langu halitafutika. Haya ni maamuzi ya Mungu Mwenye enzi ambayo tayari yameshaamuliwa mbinguni ya kwamba atabakisha jina langu na kazi zangu katika dunia na mtu yeyote atakayesimama mbele yangu atafeli kwa fadhili ya Mwenyezi Mungu… Mungu Mwenyewe aminiweka katika nafasi hii ya kuwa walau wapinzani wananitukana na wananidhani mbaya kiasi ngapi, katika kila hali hakuna yeyote anayeweza kufuta jina langu kutoka historia ya Islam. Sio leo wala baada ya miaka arobaini au khamsini hata miaka mia kuanzia leo historia itashuhudia yenyewe ya kwamba yale yote niliyoyasema ni sahihi au sio sahih, ingawa mimi sitakuwepo muda ule; lakini wakati historia ya Islam na Ahmadiyyat itaandikwa, ndipo mwanahistoria mwislamu atalazimika kutaja jina langu. Kama atajaribu kuondoa jina langu kutoka historia, itakuwa kama ameondoa sehemu kubwa ya historia ya Ahmadiyya, na kutatokea uwazi mkubwa ambao hatapata yeyote kuujazia."

(Hotuba ya Jalsa Salana Disemba 1961)

Mwenyezi Atujalie kufuata mwongozo na mafundisho ya makhalifa wetu watukufu. Mwenyezi Mungu Amrehemu Hazrat Mirza Bashir-ud-din Mahmud Ahamad Musleh Mau'ud r.a.Mungu Atujalie uwezo kufaidika na hazina zilizopatikana katika sura ya vitabu vyake, Amin.

…Mwisho

Siku

Ai siku hiyo siku, siku iso biashara
lahaula hiyo siku, siku iso na tijara
ai toba hino siku, siku iso masihara
Siku!

Rabi siku ile siku, siku iso na rafiki
kahabwe hiyo siku, kalandawe nyenye dhiki
Ai siku hiyo siku, umwitaye haitiki
Siku!

Kilibubi ndio siku, siku iso mkombozi
Subuhana hiyo siku, siku iso muombezi
Ai siku hiyo siku, ni siku ya utelezi
Siku!

Ai siku hiyo siku, saghiri kupata mvi
Ai siku hiyo siku, ni chini hapana jamvi
Siku ni mama wa siku, mambo yamekuwa hivi
Siku!

Mahmood Hamsin Mubiru [wa Mamba]
Migigombani- Kiwalani,
Dar-es-salaam.

Sikudanganye kioo

Kioo kinashangaza, uchizi kinatutia
Jicho ukikiangaza, mwenzio tamwangàlia
Jicho kwako atakaza, nachofanya igizia
Sikudanganye kioo, uzuri kweli tabia

Ukicheka atacheka, ukilia nayelia
Kasoro atakuweka, ona hapa unadoa
Uzuri takupachika, wanja umeupatia
Sikudanganye kioo, uzuri kweli tabia.

Kioo onyesha khulka, njema iliyotabia
Kwawatu kutazamika, wapate niigizia
Sisura kudanganyika, nakiburi kikajaa
Sikudanganye kioo, uzuri kweli tabia

Mtunzi
Masihi Omary Stambuli Kisagwa

Makadiani Elimu, ndiyo hasa Islamu

Naja kwako mtamboni, nikiwa na Karatasi
Ninayo hasa maoni, wakayasome unasi
Yakae mwao vichwani, Wakiri kwa Ikhilasi

Elimu ya Makadiani, Ni Islamu halisi
Nasema ninayakini, Sio ninawasi wasi
Haya nimeyabaini, kwa hiyari si Risasi.

Watuita mitaani, Japo sijina halisi
Kwamba hao Kadiani, tupate shida nafsi
Na ya mola wetu Dini, isipate uhalisi.

Kwa sababu Kurani, yafasiriwa halisi
Na ile hasa tayari, inapewa nafasi
Pale uliposhakani, kuuliza si nuksi.

Ukijiweka pembeni, visa vya Abunuwasi
Ndio viwe sikioni, Shekhe asema kwa kasi
Huku hanayo yakini, ni nini chanzo halisi

Mwanga hasa wa Dini, tumepata kwa Qudusi
Masihi wa akherini, kaja hasa kihalisi
Amezidisha yakini, kwa wasio na uasi.

Kalamu naweka chini, Naiomba Ikhilasi
Anijalie Manani, Mola aliyemkwasi
Wasiwasi wa Moyoni, Uwaondoke Waasi.

Hassan Sango
Jang Muqadas kwenye karatasi.

Maadhimisho ya Ukhalifa yafana Mkoani Ruvuma

...Kutoka toleo lililopita

Ahadi za ukhalifa katika Hadithi za Mtume[saw]

ثُمَّ تَكُونُ خِلَافَةٌ عَلَى مِنْهَاجِ النُّبُوَّةِ

Yaani ''Kisha utapatikana Ukhalifa chini ya msingi wa Unabii.

[Musnad Ahmad Jalada la 4 UK,273. Pia Mishkaat baaab Indhaar wa Tahdhiir]

Haya ni maneno matukufu mno na ilikuwa ni lazima yatimie na kwa hakika yametimia hasa juu ya Imam Mahdi a.s kwani Masihi aliyeahidiwa a.s amefafanua katika kitabu chake kiitwacho "Kuondoa kosa moja" kuwa yeye ni Nabii, hivyo basi Ukhalifa wake unaungana kabisa na kauli ya Mtume Muhammad saw kuwa utakuwepo ukhalifa ambao msingi wake upo chini ya unabii.

Mtume saw aliulizwa juu ya zama za mwisho na akajibu katika hadithi ifuatayo kuwa''

قَالَ تَلْزِمَ جَمَاعَةَ الْمُسْلِمِينَ وَإِمَامَهُمْ

Jiunge na jamaat yenye Imam

قُلْتُ فَإِن لَمْ يَكُنْ لَهُمْ جَمَاعَةٌ وَلَا إِمَامٌ

Akasema muulizaji kama hakuna Jamaat wala Imam

قَالَ فَاعْتَزِلْ تِلْكَ الْفِرَقَ كُلَّهَا

Akajibu Mtume[saw] achana na makundi yote.

[BUKHARI KITAABU MANAAQIB, NA MISHKAAT BAAB FITNAH]

Ikumbukwe ya kwamba ni Amri ya Mtume[saw] kujiunga na Jumuiya yenye Imam mmoja na kama hakuna Jumuiya yenye imam mmoja basi tumekatazwa tusijiunge na kundi linguine lolote [yaani yale makundi yasio na Imam mmoja duniani msiungane nayo]

Hii hadithi ni muhimu sana kwa waislam kufahamu kwamba tayari maamuzi sahihi yalishafanyika na Mtume saw mwenyewe na ndiye aliyefanya maamuzi haya yaliyo sahihi, hivyo ni wajibu wao kuangalia ni kundi lipi lenye imam mmoja duniani katika waislam na kisha kujiunga nalo wasipopata kundi hilo pia hawaruhusiwi kujiunga na kundi jingine lolote kwa mujibu wa hadithi, Lakini kwa fadhili za Mwenyezi Mungu kiongozi huyo yupo anapatikana hivyo ni swala la kufanya utafiti kidogo na kufanya maamuzi yakuwa wajiunge na Jamaat hiyo yenye kiongozi.

Makhalifa wa Kiahmadiya na ndiyo wa wakili wema wa Islam ni hawa wafuatao na majibu ya shutuma za wapinzani:-

1.Hadhrat Maulana Hakim Nurudin khalifa wa kwanza ra.
2.Hadhrat Mirza Bashirudin khalifa wa pili ra.
3.Hadhrat Mirza Nasir Ahmad khalifa wa tatu rh.
4.Hadhrat Mirza Tahir Ahmad khalifa wan ne rh.
5.Hadrat Mirza Masroor Ahmad khalifa wa tano atba

Huwa kuna zuka swali kuwa Ukhalifa wa Kiahmadiyya ni wa ukoo au kama wa kifalme wana rithishana kifamilia tu. Jawabu shutuma hizi au lawama hizi si sahihi kwasababu majibu yake yapo mawili moja lipo kwenye Quran na la pili lipo kwenye Historia. Kwanza watu hawa wamlaumu Mwenyezi Mungu kwanza kwamba kwanini alishusha Manabii watatu ndani ya nyumba moja yaani Hadhrat Ibrahim alikuwa nabii pia wanawe wawili walikuwa manabii Ishaaka na Ismaili pia Baba wa Nabii Yusuf. Mbili Makhalifa wa mtume wote ni ndugu pia kwa sababu Mtume saw alioa kwa Hadhrat Abubakar RA pia akaoa kwa Hadhrat Umar RA haijaishia hapo tu pia Hadhrat Othman RA alioa mabinti wawili wa Mtume saw alipofariki mmoja akaozeshwa mwingine hadi akaitwa Dhunnurain yaani Mwenye nuru mbili na Hadhrat Ali RA alimuoa Hadhrat Fatuma binti wa Mtume na kufanya naye kufunga undugu.

UKHALIFA USIO NA MSINGI WA UNABII HAUFANIKIWI

Kuna watu waliojitokeza kudai cheo cha khalifa lakini hawakukubaliwa na Mwenyezi Mungu kwani tunao mfano mmoja toka Ujerumani mnamo mwaka 1994 mtu mmoja aitwae CEMALEDDIN KAPLAN huyu alikuwa mwanzilishi wa kundi na alikuwa Mturuki na alijitangaza kuwa yeye ndiye khalifa. Alikuwa na wafuasi elfu kadhaa kati ya waturuki nchini ujerumani. Baada ya kifo chake mashindano ya kugombea cheo hicho yakasababisha kifo cha mfuasi mmoja na wengine kujeruhiwa na ndipo serikali ya ujerumani ikakipiga marufuku kikundi hicho na ukhalifa haukuendelea tena.

Kikundi kingine kilicho pigwa marufuku nchi zote ni HIZB TAHRIR nacho hiki kilianzishwa kwa lengo la kurudisha cheo cha ukhalifa tena katika uislam, na kilihamasisha waislam wote wajiunge nao ili ukhalifa upatikane. Kiongozi wao aliitwa ATA ABU RASHTA na mwanzilishi wa kikundi aliitwa AQI ATLDIN AL NABHANI mnamo mwaka 1954 kule Mashariki ya yerusalem Yaani Jordan. Mwanzilishi wao alitokea sehemu inaitwa Haifa, na ndiyo aliandaa katiba kwa ajili ya kumuweka khalifa katika uislam, kwa sababu alikuwa msomi wa fiqhi na alikuwa Qadhi huko Egypt. Ukhalifa wao pia haujafanikiwa au umekufa kabisa.

Pia mnamo mwaka 2014 tahe 29 mwezi wa 6 kiongozi wa kundi la Daish [yaani Dola yakiislam katika Iraqi na Shamu] yeye alijitangaza kuwa khalifa na akadai kuwa waislamu wote duniani wamtii yeye. Tangazo hili likakaribisha uadui mkubwa na vikundi vingine vya kiislam vyenye msimamo mkali kama vile Alqaida.

Tujiulize kwanza kwanini hawa wote na wengineo wote walishindwa kusimamisha tena ukhalifa basi jawabu lake ni hili kuwa ukhalifa uliyoahidiwa kuwepo hukumu yake ilishatolewa kuwa THUMMA TAKUU NUU KHILAFATAN ALAA MINHAJI NNUBUWAT yaani kisha utakuwepo Ukhalifa chini ya msingi wa unabii sasa wao wana kikataa cheo cha unabii na wana kitaka cheo cha ukhalifa basi wajue yakwamba ukhalifa hautaweza kusimama bila kuwa chini ya msingi wa Unabii. Hivyo kwanza wanatakiwa kukubali kuendelea kwa unabii ndipo baadae wapate neema hiyo ya Ukhalifa.

POINTI ZA KUKUMBUKWA NI HIZI

Khalifa anaweza kuchaguliwa na Allah moja kwa moja kama vile Hadhrat Adam a.s alivyo teuliwa na Allah alikuwa khalifa pia akawa khalifa, au ule utaratibu aliyouweka Mwenyezi Mungu ndani ya uislam kwamba anapofariki Mtume basi watu waaminifu na wachamungu wasio na tama za kidunia wanawafanywa wamchague khalifa ambaye atasimama baada ya mtume na ndivyo ilivyotokea kwani masahaba r.a walimchagua Hadhrat Abubakar r.a pindi alipofariki Mtume saw na wengine watatu waliofuata. Jambo la pili kukumbukwa ni hili kwamba Mtume saw Alishatoa bishara kuwa utakuja ukhalifa ambao msingi wake utakuwa ni unabii utakuja na sio maamuzi tu ya mtu binafsi kujichagua kuwa khalifa au kikundi fulani na ndiyo maana wale wote wanaoukataa unabii wanakuwa wamejifungia wao wenyewe mlango wa Baraka za ukhalifa.

Tukumbuke kuwa ukhalifa ulifuata baada ya mtume saw ulitabiliwa kudumu kwa miaka 30 tu nao ulikuwa chini msingi wa unabii. Na ukhalifa ule anao utabiri mtume saw hadhi yake ni ileile kuwa utakuwa chini ya msingi wa unabii na si vinginevyo, hivyo ukikataa unabii umeukataa ukhalifa na hakuna mafanikio au maendeleo yoyote makubwa ya kiimani yatakayo fanyika bila ya kutokuwa na khalifa. Ukhalifa ndani ya Jumuiya ya waislam wa Ahmadiyya, Historia yake na mtajo ndani ya maandiko ya Seyyidna Ahmad[as]

Ukhalifa ndani ya Jumuiya ya waislam wa Ahmadiyya ulianza mara baada ya kufariki Hadhrat Ahmad a.s na utaratibu wake wa uchaguzi siku hiyo ulifuatwa utaratibu uleule au Sunna ya masahaba wa Mtume saw walipomchagua Hadhrata Abubakar ra. hivyo hivyo alichaguliwa Hadhrat Maulana Hakim Nurudin r.a na baada ya hapo jambo hilo au utaratibu huo unaendelea hadi hii leo na tunae khalifa mtukufu wa tano [atba]. Historia yake ilianza mwaka 1908 mwezi wa tano tarehe 27 na ukafanikiwa kuendeleza lengo la ujaji wa Imam Mahdi a.s na kutimiza bishara ya Mtume saw kuwa utafuata ukhalifa uliyo chini ya msingi ya unabii.

Hadhrat Ahmad a.s anasema ''Enyi wapenzi kwakuwa hii ni Sunna ya Allah tangu kale ya mbili ili kuzikanyagilia mbali furaha mbili za bandia za wapinzani, hivyo haiwezekani sasa ya kuwa Mwenyezi Mungu Aache sunna yake ya zamani. Kwa hiyo msihuzunike kwa habari niliyowaambieni wala nyoyo zenu zisifadhaike, kwani hamna budi kuiona kudra ya pili vilevile. Na kuja kwake ni bora kwenu kwa sababu hiyo itadumu nanyi, nayo itaendelea bila kukoma mpaka Kiyama. Na hiyo kudra ya pili haiwezi kuja mpaka niondoke. Lakini niondokapo tu, hapo Mungu mtukufu Atakutumieni hiyo kudra ya pili itakayodumu nanyi milele kama Mungu Alivyoahidi katika Barahine Ahmadiyya. Ahadi hiyo hainihusu mimi bali yawahusuni ninyi, **kama Alivyosema kwamba Nitaishindisha Jumuiya hii inayokufuata juu ya wengine hadi Kiyama.** Basi hakuna budi mfikiwe na siku ya mimi kuagana nanyi ili baadaye iwadie ile siku iliyo siku ya ahadi ya kudumu. Mungu wetu huyu ndiye Mungu Atimizaye ahadi, Mwaminifu na Mkweli. Atawaonyesheni yote Aliyoahidi. Ijapokuwa hizi ni siku za mwisho za dunia na **ndiyo zama za mabalaa mengi kushuka, lakini hakuna budi dunia hii ibaki mpaka yote hayo yatimie Aliyoniambia Mungu. Mimi nimedhihirika nikiwa kudra moja kutoka kwa Mungu, nami ndimi kudra hasa ya Mungu na baada yangu watakuwapo wengine watakaokuwa onyesho la kudra ya pili.** Hivyo basi, endeleeni kuomba mkiwa pamoja ili kuingoja kudra ya pili ya Mungu. Na yawapasa wanajumuiya wema wa kila nchi wakiwa pamoja kwamba wadumu kuomba ili kudra ya pili ishuke kutoka mbinguni na iwahakikishieni kwamba Mungu wenu ndiye Mungu Muweza. Hivyo fikirini mauti yenu kuwa karibu. Hamjui saa hiyo itawadia lini.

Na ya wapasa watu wema waliotakasika wachukue baiati kwa jina langu baada yangu. Mwenyezi Mungu Anataka kwamba wote waishio katika makazi tofauti ya ardhi wakiwa katika bala la Ulaya na Asia, wote walio na tabia njema Awavutie kwenye Umoja wa Mungu na kuwakusanya katika dini moja. Hiyo ndiyo shabaha ya Mwenyezi Mungu niliyotumwa nayo kwayo. Basi ifuateni shabaha hii, lakini kwa upole, khulka njema na kuzidisha maombi. Na mpaka asimame yeyote akipata Roho Takatifu kutoka kwa Mwenyezi Mungu nyote mfanye kazi kwa pamoja.

Na yawapasa ninyi nanyi mpate sehemu katika Roho Takatifu kwa kujitakasa nafsi zenu, kwani ucha-Mungu wa kweli hauwezi kupatikana pasipo Roho Takatifu. **Na kwa kutengana kabisa na tamaa za nafsi shikeni ile njia ya kupata radhi ya Mwenyezi Mungu ambayo hakuna njia nyembamba zaidi kuliko hiyo.** Msiangukie ladha za dunia, kwani hizo zatenganisha na Mungu; jichagulieni maisha ya uchungu kwa ajili ya Mungu. Uchamungu ambao Anauridhia Mwenyezi Mungu ni afadhali kuliko ladha Anayoikasirikia Mungu. **[alwasia]**

MUONGOZO WA UCHAGUZI

Uchaguzi wa watu hao utategemea rai ya waaminio kwa pamoja. Basi yule ambaye juu yake waaminio arobaini watapatana, huyo atapaswa kuchukua baiati ya watu kwa jina langu. Yampasa huyo ajifanye mfano kwa wengine. Mungu Amenipasha habari ya kwamba Mimi Nitainua mtu mmoja kutoka katika dhuria [kizazi] chako kwa ajili ya Jumuiya yako. **Nami Nitamchagua kwa ukaribu wangu na wahyi wangu.**

Mungu Alisema Akiniambia mimi: **Taqwa (uchaMungu) ni mti unaopaswa kupandwa moyoni.** Maji yale yakuzayo ucha-Mangu ndiyo yanayonyesheleza bustani nzima. **Ucha-Mungu ni mzizi ambao kama haupo, basi hamna chochote wala lolote, lakini kama huo umebaki, basi kila kitu kipo salama**.

Lakini Mwenyezi Mungu Haitimizi kazi hii kikamilifu kwa mkono wao [manabii], bali kwa kuwafisha katika wakati ambao kidhahiri huwa na hofu ya ushinde, Huwapa wapinzani nafasi ya kucheka na kudhihaki na kufanya masihara na kuaibisha. **Na pindi wanapokwisha kudhihaki, hapo Huonyesha mkono wa pili wa kudra yake** na Huleta sababu ambazo kwa njia hiyo hutimia miradi iliyobakia kadri fulani kutimia. Ndiyo kusema kwamba Hudhihirisha kudra ya namna mbili**: (1) Kwanza, kwa mkono wa manabii wenyewe huonyesha mkono wa kudra yake. (2) Pili, katika wakati ambapo matatizo yanazuka baada ya kifo cha manabii na maadui hupata nguvu na hudhani mambo yameharibika na huwa na yakini kwamba sasa Jumuiya hii itafutika**, bali na wanajumuiya nao huhangaika na kuvunjika moyo, ***na baadhi yao wenye bahati mbaya wanashika njia ya kuritadi, hapo Mwenyezi Mungu Hudhihirisha mara ya pili kudra yake yenye nguvu na kuimarisha Jumuiya iliyokuwa inaanguka. [ALWASIA]***

1 ***Ni upi umuhimu wa kuwa na khalifa na kazi zake***

Umuhimu wa kuwa na khalifa ni huu ufuatao,

1 Umuhimu hasa wa kuwa na khalifa ni huu kuwa yeye ni nguzo ya Tauhiid yaani kuwaelekeza watu katika njia ya Allah kwa kufafanua maamrisho ya mwenyezimungu na Mtume wake na kuwaweka watu katika hali ya kumpenda mwenyezimungu na kuzidi kuwafahamisha nini wafanye katika hali ya taabu na furaha.

2 Umuhimu hasa wa kuwa na khalifa ni huu kwamba lazima katika ardhi awepo kiongozi mmoja mwenye kuamuru mema na kukataza maovu na kuwasaidia watu kumpata mwenyezimungu kwa kufuata njia za uchamungu na yeye kuwaombea kama alivyo favya Nabii.

3 Umuhimu wa kuwa na khalifa ni huu kwamba yeye ni muwakilishi wa mtume katika ardhi. Pia ili amri za kurani zitekelezeke vizuri zahitaji mtu ambae ana mawasiliano kwa wingi na Allah, zipo amri nyingi lakini ninataja mbili tu kwa haraka**, moja** kuwaondoa watu kwenye shiriki kunahitaji khalifa maana mtu wa kawaida hawezi bila ya msaada wa mwenyezimungu.

Mbili khalifa kaziyake kuwakusanya watu wachamungu walio sehemu mbalimbali ndani ya Islamu na nje ya uislam. Na ni uhakika kwamba ni watu wale tu wanao jali halizao za kiroho ndiyo wanao kusanyika na kuwa pamoja na khalifa wakitii kila amri na muongozo anao utoa tena katika hali zote za furaha na huzuni au faraja na khofu wao siku zote wapo tayari hata kuhatarisha maisha yao kwa ajili ya kutii amri za khalifa. Na watu hao wanao kusanyika kwake ni wale wanao hofia kesho akhera watakuwa na hali gani kama tutakuwa hatuna muongozo au hatuna kiongozi na tutakapo ulizwa tutajibu nini hapo khalifa huwa anawageukia watu hawa kwa huruma na mapenzi kuwaombea.

Hadhrat Masihi Maud a.s anasema kuwa '' *hakika khalifa ni kuvuli cha mtume na kwakuwa hakuna wa milele basi kunusurika kwa mwanadamu yeyote Mwenyezi Mungu mtukufu amekusuduia kuwepo kwa mitume ambao ni watukufu zaidi juu ya viumbe wengine wote katika ulimwengu, basi hali hiyo ya utume iendelezwe hadi siku ya Qiyama kwa ajili hiyo Mwnyezi Mungu alichagua cheo cha ukhalifa kiwepo ili ulimwengu uendelee kupata Baraka za Utume.*

[shahadatul Quran Rohan Khazain J.6 Ukurasa 353]

Tena sehemu nyingine Hadhrat Masih Maud a.s anasema **'' kwa kuzingatia aya ya Quran tukufu inajulikana kwamba mfumo wa ukhalifa ambao hutolewa kwa waumini kama malipo, ni mfumo uliobarikiwa sana na ni adhim sana wa uwongozi. Mfumo huu umeanzishwa kwa mikono ya Mwenyezi Mungu mwenyewe katika jumuiya ya waumini iliyo pambwa kwa vito vya imani na matendo mema au haki.** *Mwisho kwa kumalizia napenda kumuomba mwenyezimungu aendelee kutuweka ndani ya neema hii ya ukhalifa na asitupoteze baada ya kutuongoza, Ee Molawetu mkariim tunaomba Baraka na neema zako ziendelee kutushukia na utupe nguvu na imani tuzidi kutoa shukurani kwa neema hii kwani umesema ndani ya Qurani kuwa anae shukuru huzidishiwa. Molawetu utusamehe pale tulipo ghafirika na utufunike na bawa la rehma yako*

Mwisho

AHADI YA KIHISTORIA YA MWANA ALIYEAHIDIWA

Na jinsi alivyotekeleza ahadi ile

Na.
Sh. Abdul Nasir Bajwah
Jamia Ahmadiyya Tanzania

Wapo watu miongoni mwa waaminio waliotimiza ahadi waliyoahidiana na Mwenyezi Mungu , hivi baadhi yao wamekwishamaliza nadhiri zao, na wako miongoni mwao wanaongojea,wala hawakubadilika hata kidogo.(33:24)

Kwa kuomba msaada kwa Allah nitajaribu kubainisha kuhusu "Ahadi ya Mwana Aliyeahidiwa رضی اللہ عنہ (Mwenyezi Mungu Awe radhi naye)، kwa Allah سبحانہ و تعالی wakati wa kifo cha Masihi Aliyeahidiwa علیہ السلام na jinsi alivyotekeleza ile ahadi katika maisha yake yote."

Kila mwaka Tarehe 20 mwezi wa pili sisi tunasherehekea Siku ya Mwana Aliyeahidiwa na vilevile wenzetu wanajumuiya wote duniani kote mahala popote wanaendelea kuadhimisha siku hii kwa heshima na taadhima zote.

Kwa nini tunasherehekea siku hii yaani siku ya Mwana Aliyeahidiwa? Kwa nini hatuadhimishi siku zinazohusika na makhalifa wengine?

Katika kujibu swali hili Khalifa wetu mtukufu أیدہ اللہ بنصرہ العزیز تعالیansema: "Siku ya bishara ya Mwana Aliyeahidiwa tunaadhimisha ili tuweze kusisimua imani yetu na tuweze kukumbushana ile ahadi ya kwamba lengo letu haswa ni kuimarisha ukweli wa Islam na Mtume Mtukufu صلی اللہ علیہ وسلمkatika ulimwengu mzima. Siku hii sio siku ya kuzaliwa au kufariki kwake bali siku hii ni kwa kukubali dua za Masihi Aliyeahidiwa Alaih Salam. Mwenyezi Mungu Alionyesha ishara ya kwamba kutoka kizazi chake atazaliwa mtu mmoja mwenye sifa maalum na ambaye ataimarisha ukweli wa Islam katika dunia nzima, na kwa kupitia yeye njia mbali mbali zitapangwa kwa ajili ya nidhamu ya Jamaat, njia ambazo kwa kuzitumia watu watakaokuja baadae wataendelea kupata maendeleo.
Basi daima siku hii inatukumbusha kutumia nguvu zetu zote kwa ajili ya maendeleo ya Islam pamoja na kutambua majukumu yetu, na ndivyo ilivyotakiwa iwe. Sio hii tu ya kwamba tupate hadhi ya kielimu tu kwa kutambua kutimia kwa ishara hii. Mwenyezi Mungu Atujaalie uwezo."
(Hotuba iliyotolewa Tarehe 20 Feb 2009, iliyochapishwa katika Alfazl 13 Mar 2009)

"Hata kama watu watakuacha na nibakie peke yangu, nitasimama nawe na nitakabiliana na upinzani wote na mashambulizi dhidi ya ujumbe wako. "

Haya ni maneno yaliyotamkwa na Hadhrat Mirza Bashir-ud-Din Mahmud Ahmad RA wakati wa kifo cha baba yake mpendwa, Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad wa Qadian, Masihi Aliyeahidiwa na Imam Mahdi a.s.
Wakati wa kifo cha Masihi Aliyeahidiwa a.s., mtoto wake huyu alikuwa na miaka 19 tu, lakini maneno yake haya yalijawa na imani na uaminifu wa daraja la hali ya juu. Aliishi kwa miaka mingine 57 na katika umri wake wote huo kila maamuzi yake na tendo lake yalifanywa kwa kuzingatia kauli hiyo. Na kwa hiyo akatimiza ahadi aliyoitoa mbele ya baba yake na pia kwa kufanya hivyo ahadi ya Mwenyezi Mungu kwa Masihi Aliyeahidiwa a.s., kwamba atampatia mtoto atakayekuwa Musleh Mau'ud, ikatimia kwa shani na ukuu wenye kutukuka.

Baada ya kuzikwa kwa Masihi Aliyeahidiwa [as], Hadhrat Mirza Bashir-ud-Din Mahmud Ahmad r.a alirejea nyumbani kwa uvumilivu mkubwa, nyumba ambayo ilikuwa imekosa baba yake mpendwa na Imam mtukufu wa zama, ambamo hapakuwa na hazina za kidunia wala hakumrithi utawala wa kidini ya aina yoyote.
Hata hivyo, mama yake mheshimiwa Hazrat Nusrat Jahan Begum r.a aliwaambia watoto wake kwamba kwa kweli nyumba hii haikuwa tupu. Hadhrat Amma Jan [ra] (mama yake Hadhrat Sahibzada Sahib) amesema:
"Enyi Watoto! Msifikirie kwa kuangalia nyumba tupu, kuwa baba yenu ameondoka bila kuwaachia cho chote. Ameachakwa kwa ajili yenu hazina kubwa za maombi mbinguni ambazo zitaendelea kuzipatikana pamoja na fadhila za Mwenyezi Mungu na baraka zake katika maisha yenu yajayo."
Kwahivyo, hadi leo tunashuhudia kuwa kizazi cha Masihi Aliyeahidiwa a.s. kinaendelea kupata hazina zile za kimbingu katika sura ya neema ya Mungu.
Hazrat Musleh Mau'ud (ra) Katika kuzungumza kuhusu ahadi ile alisema; "Ilikuwa ni wakati wa mwisho katika maisha ya Masihi Aliyeahidiwa kabla ya kifo chake, na wanaume wengi walikuwa wamekusanyika karibu na kitanda chake, wanawake walikuwa wameshaondoka hapo.
Watu pande zote tatu walikuwa wanazunguka kitanda chake. Nilitengeneza nafasi na kusimama upande wa kichwa …
"Niliona kuwa Masihi Aliyeahidiwa a.s. alifungua macho yake, alitazama hapa na pale na kuzifunga. Tena akafumbua macho yake na alijitahidi kuangalia upande zote... Alirudia hili mara nyingi. Mwishowe alikusanya
nguvu zake zote kwa mara ya mwisho kwa sababu mtu anapokaribia kufariki anakuwa mdhaifu sana, alitazama tena pande zote,wakati macho yake yalipoona mimi….., ilionekana kana kwamba alikuwa ananitafuta mimi. Na alijisikia faraja kwa kuniona mimi. Baada ya hapo akafumba macho, na akafariki. Wakati huo nilihisi ya kwamba macho yake yalikuwa yananitafuta mimi tu. Na mimi nilifikiria kuwa haya yalikuwa matokeo ya maombi yangu mimi kutazama macho hayo kwa mara ya mwisho.
"Mara baada ya kifo chake baadhi ya watu walikuwa na wasiwasi kuhusu siku za mbele ya kwamba sasa kitatokea nini... itakuwaje kwa Jumuiya?
Ingawa nilikuwa na umri wa miaka kumi na tisa tu wakati huo, nakumbuka nilikuwa ninasimama karibu na maiti takatifu ya Masihi Aliyeahidiwa na nilisema:
'Ee Mola wangu, mimi kwa kuamini kuwa wewe ni Mjuzi wa kila kitu, naahidi kwamba hata kama wanajumuiya wote wataiacha Ahmadiyyat , mimi nitafikisha katika kila kona ya dunia ujumbe ule ambao umeudhihirisha kwa kupitia nafsi ya Masihi Aliyeahidiwa a.s."
Huzur r.a anasema; "Mtu hupitia hali tofauti tofauti katika maisha yake. Kuna hali ya uvivu, ya umakini, ya maarifa, ya ujinga, ya utii kwa Mungu na ya uzembe pia lakini hadi leo nahisi hiyo kwamba ile hali ilikuwa ya umakini wa daraja la juu na ya maarifa ya kina ya Mwenyezi Mungu kwamba kila kipande cha mwili wangu kilishiriki katika ahadi hiyo.
Nilikuwa na uhakika ya kwamba nguvu na heshima zote za ulimwengu wote hazikuwa na umuhimu wowote mbele ya dhamira, azimio na ahadi yangu ile.
Ikiwa ulimwengu ungeweza kusikia hisia na dhamira yangu bila shaka wangaliichukulia kuwa kauli ya mtu ambaye amepotea akili yake. Hata hivyo, nilikuwa na imani ya kwamba ahadi yangu hii ni jukumu langu kuu,na wakati nilipofanya ile ahadi nilikuwa najua moyoni mwangu ya kwamba ahadi hii haikuwa nje na uwezo na nguvu nilzozijaliwa na Mwenyezi Mungu."
(Fazl-e-Umar by Mujeeb-ur-Rehman, Page. 98-100)
Hazrat Nawab Mubaraka Begum r.a. binti wa Masihi Alyeahidiwa a.s. sehemu moja alisema;
Ahadi ambayo aliifanya mbele ya maiti ya Masihi Alyeahidiwa a.s, aliitekeleza kama ilivyotakiwa na msaada wa Mungu ulikuwa unaonekana katika kila hatua; Kazi zake za kuandika maelezo za Qur'an, darasa zake za Qur'an, maandishi na kauli zake, hotuba zake ni hazina kubwa na yenye thamani. Zaidi na hayo uwezo wake wa kufanya kazi yoyote, uwezo wake wa *ajabu ya* kutoa maamuzi *kuhusu mambo mbali mbali*, nia madhubuti, kuiongoza jumuiya katika kila hatua, kujenga vituo vya Islam Ahmadiyyat katika kona zote za dunia, ilhali katika kila jambo lake tunashuhudia ya kwamba Mwenyezi Mungu alimjalia Roho maalum na ya ajabu. Fadhila za Allah na Rehema zake ziliendelea kubaki naye hata adui yake hawezi kukataa kazi zake kubwa alizozifanya yeye, kijana mwenye afya dhaifu, ambaye alimdhihirisha Mwenyezi Mungu, aliwashinda wasomi na viongozi wengi wa daraja la juu.*Hazrat Khalifa-tul-Masih wa pili r.a.* aliweza kuzifanya kazi zile za ajabu ambazo Waislamu wote kwa ujumla pamoja na mali zao na elimu yao yote wameshindwa kuzifanya…
(Tarikh-e-Ahmadiyya J4, U3)
Tukiangalia athari za Kiroho na ya Kidini ya zama za Ukhalifa wake tunagundua kuwa ni ya kimataifa. Hazrat Musleh Mau'ud r.a. mwenyewe alisema;
"Mimi ni Khalifa wa Masihi Aliyeahidiwa a.s, kwahiyo mimi ni khalifa kwa ajili ya watu wa Afghanistan, Bara la Arabu, China, Japan, Ulaya, Marekani, Afrika, Samtra, Java, na Uingereza pia, yaani mimi ni Khalifa kwa ajili ya Ulimwengu mzima. Katika jambo hili watu wa Uingereza pia ni chini ya utawala wangu na hakuna nchi yoyote wa dunia ambayo sio chini ya utawala wangu wa kidini, kwahiyo hii ni amri kwa wote kuwa wafanye baiati yangu na waingie katika Jumuiya ya Masihi Aliyeahidiwa a.s.
(Tarikh-e-Ahmadiyya J4)
Basi maendeleo ya Islam ya zama hii na yajayo yatapatikana pamoja na Ukhalifa huu wa kimataifa na utawala huu ni wakidini tu. Kama alivyosema;
"Basi muda huu Mweneyzi Mungu amelazimika maendeleo ya Kiislam pamoja nami, kama daima anaambatanisha maendeleo ya kidini pamoja na makhalifa wake. Basi yule ambaye atanisikia atafaulu, na ambaye hatanisikia atafeli. Yule ambaye atanifuata, Mwenyezi Mungu atamfungulia milango ya rehema na ambaye atajitenga na mimi, atakosa rehema ya Mungu.
(Tarikh-e-Ahmadiyya J4)
Nabii kwa idhini na msaada wa Allah s.w. kwa kupitia mafundisho yake anapanda mbegu na makhalifa wake baada yake wanalinda ule mbego na wanatengeneza mazingira ambae inasaidia ule mbegu kubadilika katika mti madhubuti.
Naamini wengi wetu kwa namna moja au nyingine tunatambua kazi ya kulima, mkulima kabla ya kupanda mbegu anaandaa Ardhi, kama ardhi inakuwa ngumu anapalilia, anakatua, na kusawazisha, tena kama ardhi inakosa nguvu anachanganya mbolea, kisha anapanda mbegu. Wakati mbegu imeshapandwa, muda ule ni muda wa kuwa makini zaidi, hali ile inakuwa dhaifu mno. Vilevile baada ya kifo cha Masihi Aliyeahidiwa a.s. hali ya jumuiya ilikuwa dhaifu sana, fitna ya wale waliokuwa wanapinga Ukhalifa, uchochozi wa wapinzani na pia uchache wa idadi ya waaminio; Musleh Maud RA mambo haya yote alikabiliana kwa ujasiri mkubwa. Upande moja aliimarisha Ukhalifa kwa kumfuata Khalifa mtukufu wa kwanza r.a, kwa kumtii, kwa kumsaidia kwa namna moja au nyingine katika kulinda ule mbegu uliopandwa na Masihi Aliyeahidiwa a.s. Na upande mwingine alitengeneza mazingira yanayofaa kwa ajili ya mbegu ule kukuwa katika sura ya mti madhubuti. Kwa msaada wa Mwenyezi Mungu aliweka msingi wa nidhamu ya ajabu ambayo inaunganisha wanajumuiya katika mnyororo moja madhubuti.
Nidhamu hii inafanana na nidhamu ya damu katika mwili wa binadamu. Upendo kwa khalifa, upendo kwa mitume ya Allah, upendo kwa dini na upendo kwa Allah, hizi zote zinatembea kama damu katika jumuiya nzima kwa kupitia Nidham-e-Jamaat.
Sasa nitajaribu kugusa baadhi ya mambo yaliyotekelezwa na Mwana huyu wa Ahadi r.a. kuanzia mwaka 1908, baada ya kifo cha Hazrat Masihi Aliyeahidiwa a.s, hadi mwaka 1914 wakati alipata cheo cha Ukhalifa ili tuweze kushuhudia jinsi alivyotekeleza ahadi yake.
Mnamo 1908 aliandika kitabu chake cha kwanza kiitwacho "Nani anaweza kuzima nuru ya watu wakweli".
Alipewa jukumu la kusimamia mambo ya Dar-uz-Ziyafat (Langarkhana). Alikusanya maoni ya watu mbali mbali kuhusu kifo cha Masihi Aliyeahidiwa a.s. yaliyochapishwa katika gazeti tofauti tofauti kisha alichapisha katika gazeti la jamaat "Tash'hiz-ul-Azhan".
Aliandika Makala kadha katika gazeti la "Tash'hiz-ul-Azhan".
Katika mwaka huo huo alianza safari za mahubiri kwa amri ya Khalifa Mtukufu wa kwanza r.a. alienda Maeneo ya "Beguwal" na alitoa muhadhara huko, kisha alienda "Kathgarh" huko akifanya mahubiri. Mwishoni mwa mwaka huo katika mkutano wa mwaka alitoa hotuba kuhusu "Kivipi tunaweza kufaulu". Mwezi wa Dec 1908 alianzisha maktaba moja katika Qadian kwa ajili ya watu.
Mnamo mwaka 1909 alienda Dehli, (kwa sasa mji huu unaitwa Dilli, na mji huu ni makao mkuu ya India). Huko akifanya mahubiri alitoa hotuba mbali mbali kuhusu "Islam na dini ya Arya", "Islam na Ukristo". Safari hii alifika Mji wa Kapurthala, Lahore, Qasoor na Feruzpur, huko kote kote alihotubia hotuba yenye shani. Badae mwaka huo huo alienda Kashmir pia.
Ndani ya mwaka huu aliandika makala kuhusu mada hizi zifuatazo;
"Ishara ya Adhabu", "Ishara Mpya (Kuhusu utawala wa mfalme wa Roma)", "Tukio moja la Ajabu", "Nabii wakike wa Kikristo", "Hijabu kutoka wanawake", "Tablihg-e-Islam", "Mwezi wa Ramadhan", "Malipo ya Hisani", "Dini ya kweli", "Wokovu-(Katika kumjibu Padre Mecmilan)",
Alitoa mhadhara katika mkutano wa mwaka wa Jumuiya ya Lahore "Majma-ul-Ikhwaan". Mhadhara moja alitoa huko Lahore katika kujibu lawama ya Padre Jawala Singh.
Na pia alihotubia katika mkutano wa robo mwaka wa Gazeti la "Tash'hiz-ul-Azhan" kuhusu mada ya "Sisi na majukumu yetu".
Mnamo mwaka 1910 mjadala Fulani ulianzishwa na baadhi ya watu, Hazrat Sh. Yaqub Ali Irfani r.a. anasema;
"Mwanzo wa mwaka 1910 mjadala ulianza kuhusu mahusiano ya khalifa na Anjuman. Muda ule baadhi ya viongozi wa Anjuman na wafuasi wao walikuwa wanadhani kuwa nafasi ya khalifa ni kama kiongozi wa chama tu, na upande mwingine wanajumuiya walikuwa na imani ya kwamba Khalifa-tul-Masih ni dhihirisho la kwanza ya kudra ya pili. Wakati huo ulikuwa ya mitihani kwa ajili ya Hazrat Mirza Bashir-ud-din Mahmud Ahmad r.a, lakini huyu alionyesha ikhlaas na uaminifu wa hali ya juu, na alionyesha kwa vitendo vyake ya kwamba kitu kinachounganisha kaumu pamoja ni Khalifa pekee…"
Mnamo mwezi wa pili 1910 alianzisha darasa la Quran tukufu bada ya sala ya Maghrib, watu walishuhudia kiwango cha elimu yake ya hali ya juu na upendo wake kwa ajili ya Qur'an tukufu.
Mkutano wa mwaka wa 1909 ulifanyika mwezi wa Machi 1910, ambamo pia alihotubia.
Katika mwaka huo huo alianzisha kambi ya malezi kwa ajili ya vijana.
Tarehe 24 Mwezi wa julai 1910 Hazrat Khalifa wa kwanza r.a. alienda mji wa Multan, na alimteu Hazrat Sahibzada sahib r.a. kuwa Amir wa Qadian nyuma yake. Hivyo alihotubia hotuba ya Ijumaa kwa mara ya kwanza.
Mwezi ujao Mwezi wa nane mwaka 1910 Hazrat Khalifa wa kwanza r.a. pia alisali sala ya Ijumaa nyuma yake.
Kuanzia mwaka 1910 hadi Mar. 1914 alitumikia kama msimamizi mkuu wa Madrasa Ahmadiyya.
Wakati Hazrat Khalifa wa kwanza r.a. alipata ajali ya kudondoka kutoka kwa farasi, watu wa Anjuman alimwambia ashike nafasi ya Khalifa, lakini Hazrat Mirza Bashir-ud-din r.a. alikataa kwa ujasiri mkubwa.
Makala tofauti tofauti aliendelea kuandika katika gazeti la Tash'hiz-ul-Azhan. Aliandika kuhusu "Tofauti kati ya manabii na wanajimu", "Falsafa ya Wokovu", "Ishara ya Kimbingu", "Kuweka mbele dini kuliko dunia".
Mnamo mwaka 1911 Hazrat Maulawi Sayyid Muhammad Ahsan r.a wakati alipokuwa anatoa hotuba ya Ijumaa katika msikiti wa Aqsa Qadian alitoa ushahidi ya kwamba Hazrat Mirza Bashir-ud-din r.a. ndiye aliyezungumzwa katika tangazo la bishara ya Musleh Mau'ud.
Mwaka huo huo kwa kupata idhini ya Khalifa wa kwanza r.a. yeye alianzisha Majlis Answarulla.
Aliandika Makala moja kuhusu "Khaatam-un-Nabiyyin" katika gazeti la "Nizam-ul-Mashaaikh-Dehli".
Mnamo May-1911: Alitoa hotuba mbili katika mkutano wa mwaka wa Anjuman Ahmadiyya Batala kuhusu mada ya "Dhehbu la kweli ni lipi" na "haja ya Imam".
Mwezi wa Juni 1911 alienda maeneo ya Dilhozi kwa kufuata mwongozo wa Khalifa Mtukufu wa kwanza r.a. Huko alionana na Padre Yungson. Aliongea naye kuhusu etikadi la kikristo "Utatu". Badae ilichapishwa kwa jina la "Pahari Wa'az" yaani "Nasaha ya Mlimani".
Alitoa Hotuba ya Eid-ul-Fitr katika mwezi wa Sep 1911.
Katika mwaka huu pia aliendelea kuandika makala mbali mbali katika gazeti la Tash'hiz-ul-Azhan, kwa mfano aliandika kuhusu "Firaun wa Mussa a.s.", Mwislamu ni yule tu ambaye anawaamini mitume wote", "Mazoea ya kula nyama", "Maoni juu ya kitabu cha mabaniani Sathiarath Parkash", "Kutimiza Ahadi", "Sisi tunamfahamu Mirza Sahib kuwa nani" na "Siku za Krismasi"
Alitoa hotuba katika mkutano wa mwaka 1911 kuhusu "Madaraja ya Taqwa".
Mnamo 1912: Alitoa hotuba katika mahafali ya Madrasa Ahmadiyya. Mwaka huo huo alianza safari ya madarasa mbali mbali ya India ili mambo yanayohusika na Madrassa Ahmadiyya yaboreshwe. Katika mwaka huu alisafari ya Misr na nchi ya Arabu,pia Alifanya hija. Mwanahabari mmoja alitoa maoni yake kumhusu yeye akiwa alisema;
"Nilifurahi sana kwa kuonana na Sahibzada Bashir-ud-din Mahmud Ahmad sb. Huyu ni mwenye khulka njema sana… Naweza kusema anaye ufahamu mkubwa wa mambo mbali mbali."
Mwaka huu alisafiri na Khalifa wa kwanza r.a. kwenda Lahore na katika hotuba yake aliwahimiza vijana kujifunza lugha ya Kiarabu. **Mnamo mwaka 1913** katika mwezi wa Juni alianzisha gazeti la "Al-Fazl".
Katika gazeti la "Tash'hiz-ul-Azhan" aliandika makala kuhusu "hoja za uwepo wa Allah" na "Adhma ya Masihi kutoka katika Qur'an".
Mwezi wa Jul 1913 Aliihotubia Mkutano wa Answarullah. Aliendelea na mihadhara na mahubiri katika Shimla, Gujranwala na Multan. Katika Jalsa Salana alitoa hotuba kuhusu "Namna za kupata uchamungu"
Mnamo mwaka 1914 Alianzisha mfungo wa "Dawat ila-al-Kher" kwa ajili ya mahubiri.
Alisafari maeneo ya Lodhi Nangal, Chakwal na Wazirabad. Tarehe 13 Mar 1914 alitoa nasaha kwa wanajumuiya katikia hatoba ya Ijumaa ya mara ya mwisho kabla ya kuchaguliwa Khalifa na alisema;
"Mweneyzi Mungu Huwasaidia waja wake katika hali ngumu kwa namna ya ajabu, kama kuna dhati ambaye anaweza kumsaida mtu katika msiba fulani au hali ngumu, huyu ndiye Allah pekee. Anaweza kutoa shida zote. Ukienda kwa yeyote kwa kumuacha Mungu, basi ukumbuke wewe ni mshirikina. Ndipo geukeni kwake tu na tegemeeni Mungu tu, ili Awasaidie katika shida yenu hii. Uwezo wa kuomba dua pia tunapata kwake tu. Mungu Atujalie kuomba maombi yale yanayokubalika na Atuongoze kwenye njia iliyonyooka". (Tarikh-e-Ahamdiyyat J4-Pg94)
Hii ndio siku ambamo Khalifa wa kwanza r.a. Hazrat Hakeem Maulawi Nur-ud-Din sahib Bherawi r.a. alifariki. Mara Hazrat Sahibzada Sahib r.a. alimaliza hotuba ya Ijumaa alielekea kumuona Khalifa wa kwanza r.a. lakini alikuwa njiani huko alipata taarifa ya kufariki kwake. Alihuzunika sana kwa kuondoka kwa mpenzi wake, kiongozi wake na mwalimu wake.
Kipindi kile kilikuwa ngumu sana kwa ajili ya wanajumuiya wote, ingawa alikuwa hana tamaa ya kuchaguliwa Khalifa na alijitahidi kwamba yeyote mwingine achaguliwe, lakini waaminio wengi ambao walikuwepo Qadian kwa matakwa ya Mwenyezi Mungu walifanya baiati yake, takriban watu elfu 2 na mia tano na walikuwa watu hamsini tu ambao hawajafanya baiati muda ule.
Waaminio wenzangu! Leo sisi ni mashahidi wa jambo hili ya kuwa nani alikuwa anafuata haki, wale ambao walikataa Ukhalifa au wale ambao walifanya baiati siku ile. Msaada wa Allah unadhihirisha ukweli wazi wazi. Leo tukiwa hapa katika nchi ya Afrika Mashariki tunaendelea kumkumbuka yule Mwana wa Ahadi ambaye mwenyewe alisema
Utafika wakati ambapo watu watasema, Mwenyezi Mungu Amrehemu mpenzi huyu wa Ummati huu.

Leo duniani nzima watu wanaendelea kutoa ushahidi ya kuwa huyu huyu Mwana wa ahadi ni Musleh

Endelea Uk wa 6..

MATUKIO KATIKA PICHA





Pichani ni Sadr Sahiba Bi. Zena Nyange, pamoja na Majlis Lajna na waliowahi kuwa Masadr Lajna wa Tanzim



Pichani ni Nasratul Ahmadiyya wakisoma Shairi kwa pamoja katika sherehe za Karne.



Pichani ni Sadr Majlis Khudamul Ahmadiyya Tanzania, Mh. Rahim J. Mwanga Sahib akiwahutubia Khudam na Atfal katika vikao vya Ijtimaa ya 33 Kitaifa, Kitonga Jijini Dar es Salaam.

Kalamu kutoka Kanda ya Ziwa

...Kutoka tolro lililopita

KUCHANUA KWA CHEMCHEM YA JAMAAT AHMADIYYA MKOANI SHINYANGA - 6



Yousuph Mgeleka (Muijukuu)

Enyi ndugu zangu wapendwa,
Zipokeeni neema za Jumuiya ya Waislamu Ahmadiyya kutoka Ukanda wa Ziwa. Zitambueni zama ambazo Allah ameijaalia Jamaat Ahmadiyya na kupokelewa kwa upana wake kutoka Ukanda wa Ziwa. Alhamdulillah kwa fadhila zake Allah, zama hizi tumejaaliwa neema ya Jamaat Ahmadiyya kupokewa kwa mapana katika mikoa ya Shinyanga, Simiyu na Geita. Hii ni neema kutoka kwa Allah, neema ambayo hatupaswi kuibeza hata kwa hatua moja. Neema ambayo wale wazee wetu wa mwanzo kuipokea Jumuiya nchini, walitamani kuziona neema hizi katika uhai wao. Neema ambazo daima tutazikumbuka.

Enyi ndugu zangu wapendwa,
Naomba tuzitambue neema hizi adhwiim alizotuteremshia Allah katika zama zetu. Allah ametujaalia neema ya sisi kuwa ni wanajumuiya ndani ya nchi yetu Tanzania, huku Allah akiuonyesha ulimwengu namna ambavyo neema ya kupokelewa Jumuiya inavyoshamiri katika ukanda wa Ziwa. Neema ambayo hata nchi majirani zetu wangetamani neema hii iwe nao na kushuhudia ukweli wa Masih aliyeahidiwa. Nawaomba sote tusizibeze neema hizi ambazo tunazishuhudia katika neema ya uhai wetu.

Enyi ndugu zangu wapendwa,
Kwa zaidi ya miaka 50 iliyopita, sote tunatambua kuwa ukanda wa Ziwa ulipata neema za kuhudumiwa kijamaat na wabashiri mbalimbali ambao ni babu zetu, na hata baba zetu, ama sisi wenyewe. Sote tunatambua jitihada kubwa walizozifanya masheikh mbalimbali na waalim mbalimbali katika ukanda wa Ziwa, bali juhudi kubwa zilizofanywa na wanajumuiya wachache kutoka ukanda huu huku wakitanguliza uvumilivu na subira katika kuufikia ufaulu wa Jamaat Ahmadiya. Sote tunafahamu walikuwepo viongozi wetu mbalimbali (Amir wa nyakati husika) waliojaaliwa kututembelea miaka mingi iliyopita, lakini jitihada zote za viongozi wetu hao Allah alijaalia subira ili zama nyingine zije na ateremshe neema zake, neema zilizoambatana na kuzinyoosha nyoyo na nafsi za wananzengo wa Ukanda huu. Matokeo yote tunayoyaona kutoka ukanda wa Ziwa, ni mpango maalum wa Allah na nyakati husika. Basi tutambue na tuwe na yakini thabiti kwa mafanikio yanayoendelea kupatikana ukanda wa Ziwa.

Enyi ndugu zangu wapendwa,
Jitokezeni. Naam jitokezeni kwa makundi na kifua mbele kuja kutusaidia kufanya malezi kwa wanajamaat wengi wapya waliopo. Jitokezeni kwa kupishana kundi hili dhidi ya jingine, yaani Lajna kwa Khuddam, Ansaar kwa Twifl na Nasratul Ahmadiyya. Sogeeni karibu nasi ili tushirikiane kuifanya dini yetu tukufu ya Islam ikishika hatamu, bali sogeeni muache alama njema ya kufundisha Qur'an kwa walau "Alif". Sogeeni na muwe karibu mtusaidie kufundisha "Nguzo za Imaan na Nguzo za Kiislamu". Sogeeni mtusaidie kuwafundisha viumbe wa Allah wenye kiu ya kuabudu ili wajue kusali. Na sogeeni ukanda wa Ziwa mje mtusaidie kuwafundisha wanajamaat namna ya kushika udhu na namna ya kujisafisha na kujitakasa. Sogeeni kuja kutusaidia huku mkiwa na yakini kuwa, kwa kazi zote na muda mtakaotumia huku, basi malipo mtayapata mbele ya Allah baada ya maisha yetu mafupi hapa duniani. Leo tunamkumbuka Mcha Mungu marehemu Mzee Mohamed Namwete aliyejitoa muhanga na kuja mkoani Shinyanga na kupanda mbegu za Islam Ahmadiyya, hatunae duniani waila anajichumia thawabu mema kwa kuja kuzinusuru nafsi za makundi ya wanoujiunga na Jamaat Ahmadiyya Ukanda wa Ziwa.

Enyi ndugu zangu wapendwa,
Duniani ni mapito tu, tena tumejaaliwa neema ya maisha mafupi mno. Tumeaswa kuitanguliza dini mbele ya dunia. Heshima zetu zipo katika kumtumikia Rahman, hapo ndipo Allah atatujaalia heshima hapa duniani na aakhera Insha Allah. Nafasi na fursa njema ndio hii katika zama zetu, tusikae vivulini na kunong'ona koridoni huku tukinyoosha vidole kwa wale wajitoleao kuhubiri na kulea wanajamaat wapya. Njooni, njooni, njooni kwa wingi huku bara tulipo. Hizi ni zama ambazo huenda tukazijutia iwapo zikitupita, na ikabaki historia tu. Tunawaita mkaribie ukanda wa Ziwa nanyi mchangie kumwagilia maji kwenye mbegu ambazo zimepandwa, tutarajie malipo yetu ni kutoka kwake Allah Sub'hanahu wa ta'ala pekee.

Enyi ndugu zangu wapendwa,
Tutafakari kwa udhati wa kazi za Jamaat Ahmadiyya ukanda wa Ziwa, kazi ambazo ni fursa kwa kila Muahmadiyya nchini. Msibaki nyuma, bali jitokezeni kuzikimbilia neema hizi. Endesheni harambee za nauli huko matawini mlipo, mpate nauli na mje kuwahudumia viumbe wa Allah, mziokoe nafsi hizi. Huku mtashukuriwa kwa Alhamdulillah nyingi nyingi, na Jazaakumullah nyingi (ambazo hazipotei na mtazikuta baada ya maisha ya duniani). Basi utazameni mlango huu ulio wazi kwetu, mlango ambao upo wazi na twaushuhudia katika zama za uhai wetu.

Enyi ndugu zangu wapendwa,
Je, hivi ni kweli kazi hizi kubwa za malezi tulizonazo Ukanda wa Ziwa ziendelee kusubiria wanaadam na wanajamaat wenzetu watoke ughaibuni kuja kutusaidia malezi? La hasha! Basi shime tujitokeze, na tujitokeze kuzitafuta rehma zake Allah. Bali tujitokeze kuja kuwasaidia malezi makubwa masheikh na waalimu wetu huku. Njooni tuyaokoe matawi ambayo wanashindwa kumpata Imaam ili kuwaongoza kusali Ijumaa, njooni tuzinusuru nafsi hizi kuzitoa gizani na kuzileta kwenye nuru. Nawaomba kwa unyenyekevu mkubwa mje mtusaidie kuwahurumia hawa viumbe ambao sote tunafahamu wametoka kwenye ombwe lipi, wametoka kwenye giza lipi. Nawaomba tutenge neema ya pumzi zetu walau kwa siku 3 na mje mpande mbegu ya kuziokoa nafsi hizi za wanajamaat waliojiunga na wanaohitaji elimu.

Enyi ndugu zangu wapendwa,
Mimi kiumbe mwenzenu naishia hapa kwa leo, kwani kila Mwanajamati ni Mwalimu kwa mwenzake. Na ukumbusho mwema humfaa muaminio. Kwa machache niliyonena mimi kiumbe mwenzenu dhaifu, sasa natia nanga. Naimani mbiu njema nimeipaza na mmeisikia. Namuomba Allah azifungue bongo na nyoyo zetu, namuomba Allah atuhurumie sote. Aamin.

Itaendelea.... Inshallah toleo lijalo

Mtume Mtukufu (saw): Mfano Mkuu

Kutoka uk. 12

Hudhur (atba) alisema kwamba masahaba walipigana kwa ushujaa mkubwa. Mtume Mtukufu (saw) aliwaambia masahaba zake kwamba yeyote yule ambaye atapigana kwa subira na hatageuza mgongo ataingia Peponi. Hadhrat Humam (ra) alionyesha mshangao wake na kujiuliza, 'Je, kizuizi pekee kati yangu na Pepo ni kuuawa na watu hawa?' Baada ya haya, akachukua upanga wake na akapigana kwa ushujaa hadi akauawa kishahidi.

Abu Jahl Yuaanguka Vitani:

Hadhrat Khalifatul Masih wa Tano (atba) alisema kwamba Hadhrat Abdur Rahman bin Auf (ra) anasimulia kwamba wakati wa Vita vya Badr, alitazama kushoto na kulia kwake na akaona wavulana wawili wadogo wamesimama kando yake. Aliwaza jinsi wawili hawa wataweza hata kumlinda. Mmoja wa vijana wale alimnong'oneza na kumtaka amwelekeze Abu Jahl ili amuuwe au auwawe katika mchakato huo. Kisha, mvulana mwingine upande ule mwingine akamnong'oneza na kumuuliza jambo lile lile. Alimuashiria Abu Jahl kwa wote wawili. Walikimbia kama umeme kuelekea kwa Abu Jahl ili kumuua. Wawili hawa walikuwa Mu'adh na Mu'awwidh. Mmoja wao alipoteza mkono wake katika juhudi hii.

Hudhur (atba) alisema kwamba baada ya vita, Mtume Mtukufu (saw) alimtafuta Abu Jahl lakini hakumpata. Mtume Mtukufu (saw) alimuombea asiepuke. Mtume Mtukufu (saw) kisha akaagiza atafutwe Abu Jahl. Hadhrat Abdullah bin Mas'ud (ra) hatimaye alimkuta Abu Jahl katika hali ya kuwa yu hai. Abu Jahl aliuliza kama wamemuuwa mtu yeyote mwenye heshima zaidi kuliko yeye. Kisha akauliza ni nani aliyeshinda vita. Abu Jahl bado alikuwa akimdhihaki Hadhrat Abdullah bin Mas'ud (ra); hata hivyo, alimuua na kisha akampelekea Mtume Mtukufu (saw) kichwa chake ambapo Mtume Mtukufu (saw) alimtukuza Mwenyezi Mungu. Kwa mujibu wa riwaya nyingine, Mtume Mtukufu (saw) alikwenda mahali ambapo Abu Jahl aliuawa. Imeandikwa kwamba Mtume Mtukufu (saw) alisema kwamba kila umma una Firauni na ya kwamba Firauni wa umma wake alikuwa Abu Jahl.

Hudhur (atba) alimnukuu Hadhrat Khalifatul Masihi wa Pili (ra) aliyesema kwamba hata matakwa ya mwisho ya Abu Jahl hayakutimizwa. Wakati huo, ilikuwa ni desturi kwamba ikiwa chifu wa Makka aliuawa, kichwa chake kingekatwa kutoka sehemu ya chini ya shingo ili aweze kutambulika. Hata hivyo, Abu Jahl alipoeleza matakwa haya Abdullah bin Mas'ud (ra) hakuyatimiza.

Hudhur (atba) alimnukuu Hadhrat Mirza Bashir Ahmad (ra) anayeandika:

'Kwa hivyo, wawe Muhajirina au Ansari, wote walipigana kwa ushujaa na ikhlasi. Walakini, idadi ya maadui na uwezo wao katika vifaa ulionekana kuwa nguvu isiyoweza kushindwa, na matokeo ya vita yalibaki kuwa ya utata kwa muda. Mtume Mtukufu (saw) alikuwa akijishughulisha na dua za dhati, na uchungu wake uliongezeka muda baada ya muda. Hata hivyo, hatimaye, baada ya muda mrefu sana, Mtume Mtukufu (saw) alisimama kutoka kwenye sijda na kutoka nje ya hema huku akisoma bishara ifuatayo ya kimungu:

"Jeshi la Maquraish bila shaka litashindwa na kuonyesha migongo yao katika kukimbia."'

(The Life & Character of the Seal of Prophets (sa), Juzuu 2, uk. 153).

Hudhur (atba) alimnukuu Hadhrat Mirza Bashir Ahmad (ra) zaidi anayeandika:

'Akitoka nje ya hema lake, Mtume Mtukufu (saw) alipitisha macho katika pande zote nne na kukuta uwanja wa vita ulikuwa na umwagaji wa damu. Wakati huo, Mtume Mtukufu (saw) alichukua gao la mchanga na kokoto na kuzirusha upande wa makafiri, na akasema kwa nguvu, "Nyuso zao na ziharibike." Kisha, Mtume Mtukufu (saw) akawaita Masahaba kuanzisha mashambulizi ya ghafla. Wakati sauti ya Bwana wao Mpendwa ilipofikia masikio yao, waliinua kauli mbiu ya Ukuu wa Mwenyezi Mungu, na kusonga mbele kwa shambulio la papo hapo. Kwa upande mwingine, Mtume Mtukufu (saw) alikuwa ametoka tu kurusha gao la mchanga wakati upepo mkali ulipoanza kujaza macho, midomo na pua za makafiri na kokoto. Mtume Mtukufu (saw) amesema: "Hili ni jeshi la Malaika wa Mwenyezi Mungu waliokuja kutusaidia kwa msaada wa Mwenyezi Mungu. Katika baadhi ya masimulizi, imesimuliwa pia kwamba wakati huo, baadhi ya watu waliwaona hata malaika hao. Vyovyote iwavyo, watemi kama vile 'Utbah, Shaibah na Abu Jahl, walikuwa tayari wamechanganyika na udongo. Kwa matokeo ya shambulio hili la ghafla la Waislamu na upepo mkali wa ghafla, Maquraishi walianza kuishiwa nguvu, na hofu ikazuka haraka katika jeshi la Maquraishi. Uwanja wa vita uliondokewa (na maadui) kwa muda mfupi tu.'

(The Life & Character of the Seal of Prophets (sa), Juzuu 2, uk. 153-154).

Msaada wa Mwenyezi Mungu kwa Ajili ya Waislamu:

Ilikuwa ni katika tukio hili ambapo Mtume Mtukufu (saw) alitupa kokoto sawa na ufunuo wa Mwenyezi Mungu.

وَمَارَمَيْتَ اِذْرَمَيْتَ وَلٰكِنَّ اللّٰهَ رَمٰى۔

'Na hukutupa wewe ulipotupa, walakini Mwenyezi Mungu ndiye Aliyetupa.'

(Surah Al-Anfaal, 8:18).

Hudhur (atba) alisema kwamba Mwenyezi Mungu Anasema katika Qur'ani Tukufu,

نَمِّدُكُمْ بِاَلْفٍ مِّنَ الْمَلٰٓئِكَةِ مُرْدِفِيْنَ وَاِنْ تَصْبِرُوْا وَتَتَّقُوْا يَاْتُوْكُمْ مِّنْ فَوْرِهِمْ هٰذَا يُمْدِدْكُمْ رَبُّكُمْ بِخَمْسَةِ اٰلٰفٍ مُّسَوِّمِيْنَ

'(Kumbukeni) mlipokuwa mkiomba msaada kwa Mola wenu, naye Akawajibuni: Kwa yakini Mimi Nitawasaidieni kwa Malaika elfu moja wafuatanao mfululizo.'

(Surah Al-Anfaal, 8:10).

Hudhur (atba) alisema kwamba Mtume Mtukufu (saw) alishuhudia kuwepo kwa Malaika walioshuka wakati wa vita. Siku ya Badr, Mtume Mtukufu (saw) alimuashiria Malaika Jibril akiwa amepanda farasi. Imeandikwa kwamba Malaika Jibril alimwendea Mtume Mtukufu (saw) na kumuuliza ni daraja gani angewapa Waislamu walioshiriki katika Vita vya Badr. Mtume Mtukufu (saw) alisema kwamba wao ni bora zaidi katika Waislamu. Jibril akajibu kwamba hivyo pia malaika ni bora walioshiriki katika Vita vya Badr. Hata watu wa Makka waliokufuru walishuhudia kwamba waliona viumbe weupe wakipanda farasi na kupigana vitani. Masahaba wengine wamesimulia kwamba siku ya Badr, kupambanuka kwa Malaika ni kwamba walikuwa wamevaa vilemba vyeupe. Hudhur (atba) alieleza kwamba pale ambapo baadhi ya watu wanafikiri kwamba hii ilikuwa ni habari njema tu ya msaada na malaika hawakushuka kweli kweli, masimulizi ya kweli yanaonyesha wazi kwamba malaika walishuka wakati wa vita kwa namna ya maono ambayo hata makafiri waliyaona.

Hudhur (atba) alimnukuu Hadhrat Masihi Aliyeahidiwa (as) alieyeeleza kwamba katika hekima isiyo na kikomo ya Mwenyezi Mungu, Aliwafanya maadui waonekane wachache kwa Mtume Mtukufu (saw) katika ndoto ili Waislamu wasipoteze matumaini tangu mwanzo. Vile vile, katika njozi, Mwenyezi Mungu Aliwafanya malaika waonekane maelfu wakati wa Vita vya Badr ili kuongeza imani ya Waislamu na ili wajue kwamba hawakuwa peke yao.

Hudhur (atba) alisema vita viliisha na Waislamu kwa hakika wakawa washindi. Katika vita hivyo, Waislamu 14 waliuawa kishahidi huku watu 70 wa Makka wakiuawa, wengi wao wakiwa wakuu wa Makka.

Hudhur (atba) alisema kwamba ataendelea kusimulia matukio haya katika siku zijazo.

Maombi kwa Umma wa Kiislamu:

Hadhrat Khalifatul Masih wa Tano (atba) alisema kwamba alitaka kukumbushia kwenye maombi maalum. Hudhur (atba) alisema tunapaswa kuwaombea Waislamu huko Palestina; Mwenyezi Mungu Awafanyie wepesi na Awasaidie wale wanaodhulumiwa. Na Awape uongozi ule unaotimiza haki zao, unaowaongoza, na unaojaribu kukomesha ukandamizaji wao. Wameonewa sana, na inaonekana kana kwamba hakuna mtu wa kuwasaidia. Lau Waislamu wangeungana basi mambo hayo yangeweza kuepukika.

Hudhur (atba) alisema vivyo hivyo, huko Sweden, na katika nchi zingine ambazo watu wamepewa uhuru wa kutenda wakatavyo kwa jina la uhuru wa kujieleza na kusema, wanaumiza hisia za Waislamu. Wanaivunjia heshima Qur'ani Tukufu au kutoa lugha za dharau dhidi ya Mtume Mtukufu (saw). Hudhur (atba) alisema kwamba hii pia ni kwa sababu ya mfarakano baina ya Waislamu. Hata wakiinua sauti zao, huwa ni kwa muda tu na tena haifai kabisa.

Hudhur (atba) alisema kwamba Waislamu pia wanalengwa nchini Ufaransa, lakini mwitikio wa Waislamu pia sio sahihi. Machafuko na uporaji hautafanikisha chochote. Waislamu lazima watengeneze matendo yao kulingana na mafundisho ya Kiislamu. Ni pale tu maneno na matendo yao yanapowiana na mafundisho ya Kiislamu ndipo watakapoona mafanikio.

Hudhur (atba) alisema tunachoweza kufanya ni kuomba, hasa kwa ajili ya ulimwengu wa Kiislamu, na kwa ajili ya ulimwengu mzima kwa ujumla; Mwenyezi Mungu amlinde kila mtu dhidi ya ukatili na amani itawale duniani. Kila mtu aelewe umuhimu wa kutimiza haki za mwenzake. Vinginevyo, ulimwengu unaelekea kwenye uharibifu mkubwa. Mwenyezi Mungu Arehemu.

Hudhur (atba) alisema pia kuwaombea hasa Waahmadiyya walioko Pakistani, kwamba Mwenyezi Mungu Awahifadhi na shari zote.

Hudhur (atba) alisema kwamba huko Ufaransa, kuna maandamano mengi, na inasemekana kwamba mengi yanafanywa kwa ajili ya kijana aliyeuawa, lakini kwa kweli hii haionekani kuwa kweli. Uchangishaji wa pesa uliofanywa kwa ajili ya mvulana huyo umefika Euro 200,000 pekee, ambapo kwa afisa wa polisi aliyefungwa, zaidi ya euro milioni moja zimekusanywa. Mwenyezi Mungu pekee ndiye Anayeweza Kuwarehemu, Kuwawezesha watu hawa kufanya uadilifu, na Kuwawezesha Waislamu kuungana.

The First Muslim Newspaper in Swahili Language since 1936

Ahmadiyya Muslim Jamaat Tanzania

Mapenzi ya Mungu

MAPENZI KWA WOTE BILA CHUKI KWA YEYOTE

Mtume Mtukufu (saw): Mfano Mkuu

Matukio ya Vita vya Badri

Baada Ya Kusoma Tashahhud, Tawwudh na Surah Al Fatiha Hadhrat Mirza Masroor Ahmad Khalifatul Masih wa Tano (atba) alisema kwamba katika hotuba iliyotangulia, alikuwa akieleza hofu ya Waislamu waliyokuwa nayo juu ya makafiri wa Makka, katika kipindi ambacho alieleza mzozo baina ya Abu Jahl na Utbah.

Hudhur (atba) alisema kwamba Utbah bin Rabi'ah alisonga mbele kutafuta nafasi ya kupigana na mtu mmoja mmoja. Baadhi ya vijana kutoka Ansari waliitikia mwito wake, lakini Utbah aliuliza wao ni nani. Walipomjulisha, Utbah alisema kwamba hakuwa na uhusiano wowote nao, na ya kwamba dhamira yao pekee ilikuwa ni kupigana na jamaa zao waliokuwa wametokana na Maquraishi. Alimwita Mtume Mtukufu (saw) na kusema kwamba atume watu wanaoweza kushindana nao na wale wanaotoka katika familia zao. Hivyo, Mtume Mtukufu (saw) alimuita Hadhrat Hamzah (ra), Hazrat Ali (ra) na Hazrat Ubaidah bin Harith (ra). Hazrat Hamzah (ra) alipigana na Utbah, Hazrat Ali (ra) alipigana na Shaibah, na Hazrat Ubaidah (ra) alipigana na Walid. Hadhrat Hamzah (ra) na Hazrat Ali (ra) wote walishinda, wakati Hazrat Ubaidah (ra) alijeruhiwa na Hazrat Hamzah (ra) na Hazrat Ali (ra) walikwenda kumsaidia.

Hudhur (atba) alisema kwamba wakati wa vita hivi, Hadhrat Ubaidah (ra) alipoteza mguu wake.



Hadhrat Ameerul Mumineen Mirza Masroor Ahmad Khalifatul Masih wa Tano[atba] akihutubia waumini katika Masjid Mubarak, Uingereza siku ya Tarehe 7 Julai 2023, Mtume[saw]; Mfano Bora.

Alipopelekwa kwa Mtume Mtukufu (saw) aliuliza kama atahesabiwa kuwa ni shahidi ambapo Mtume Mtukufu (saw) alijibu kwamba hakika atahesabiwa. Ilikuwa ni wakati wa kurudi kutoka Badr ambapo Hazrat Ubaidah (ra) hakuweza kuponea majeraha yake na akawa shahidi. Imesimuliwa kwamba alipopoteza mguu wake na kupelekwa kwa Mtume Mtukufu (saw), alilazwa karibu na Mtume Mtukufu (saw), na Mtume Mtukufu (saw) aliweka mguu wake uliobarikiwa chini ya Ubaidah (ra).

Hudhur (atba) alisema kwamba pande hizo mbili zilipokaribia kupigana vitani, Abu Jahl aliomba kwamba wale waliovunja uhusiano wa jamaa na wakasema mambo ambayo hakuna mtu aliyeyasikia hapo kabla waangamie. Hadhrat Masihi Aliyeahidiwa (as) alieleza kwamba labda Abu Jahl alifikiri kwamba Mtume Mtukufu (saw) alikuwa akiishi maisha machafu (Mungu-Apishe mbali) kutokana na hayo akafanya maombi haya. Hata hivyo, haikupita zaidi ya saa moja baada ya kuomba dua hii kwamba Abu Jahl mwenyewe alipoteza maisha yake vitani.

Hadhi ya Kuingia Peponi Watunzwa Mashahidi wa Badr:

Hadhrat Khalifatul Masih wa Tano (atba) alisema kwamba imesimuliwa kuwa ingawa Waislamu walikuwa wachache na walikuwa na vifaa vya chini sana, walikuwa na kitu ambacho hakuna nguvu nyingine katika ulimwengu huu inaweza kukishinda, na hiyo ni imani iliyo hai. Hili liliwaimarisha kwa nguvu isiyo ya kawaida. Walionyesha ile imani, ambayo mfano wake haujawahi kuonekana.

Hudhur (atba) alisema kwamba shahidi wa kwanza katika Uislamu alikuwa Hadhrat Mahjah (ra), mtumwa aliyeachwa huru wa Hadhrat Umar (ra) baada ya kulengwa na mshale ulioingia shingoni mwake.

Hudhur (atba) alisema kwamba kijana mmoja, Harithah bin Suraqah bin Harith (ra) aliuawa kishahidi katika Vita vya Badr. Mama yake alimwendea Mtume Mtukufu (saw) na kumuuliza kama anajua kuwa yeye alimthamini Harithah kiasi gani. Alisema kwamba ikiwa ameenda mbinguni, ataweza kusubiri. Walakini ikiwa kulikuwa na kitu chochote kinyume na hii, basi anapaswa kungojea kuona atafanya nini. Mtume Mtukufu (saw) aliuliza, 'Je, kuna pepo moja tu? Mwanao yuko Jannat al-Firdaus (kituo cha juu kabisa Peponi).

Endelea uk.11



Nakala hii itapatikana kwa Sh. 8,000/=

Je, Wajua?

Je wajua kuwa Tesla ni moja kati ya kampuni nyingi zinazotengeneza magari yajiendeshayo yenyewe kwa kutumia Kompyuta. Watu kadhaa wamekutwa wakiwa wamelala wakati gari hizo zikijiendesha zenyewe kwani ni kosa kisheria kufanya hivyo. Kampuni nyingine iitwayo Waymo inatoa huduma ya usafiri wa mjini (Taxi) katika miji kadhaa ya Marekani ambazo hazina Dereva (hujiendesha zenyewe). Ni kivutio kwa watu wengi sana kuona wakipanda Taxi na kuona ikijingoza yenyewe bila ya Dereva.

Kwa Makala, Maoni, Ushauri; Tuandikie

mapenziyamungu36@gmail.com